MID WEEK JACKPOT!
TZS. 583,071,860
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**CCM** yampa kongole Mwinyi, Chongolo aonya wanaojipitisha

UKURASA 3&5




UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Mei 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581312

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


# Mgomo wa Kariakoo ulivyotikisa serikalini

• **Waziri** Mkuu aacha kikao cha Bunge kuwawahi, atoa maagizo matatu... *Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo wakiwa nje ya maduka yao kutokana na mgomo ulioitishwa jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**SERIKALI: URAIA PACHA RUKHSA KWA WATOTO**

SERIKALI imelieleza Bunge kuwa hairuhusu uraia pacha kwa watu wazima isipokuwa kwa watoto...

UKURASA WA 4

**SERIKALI KUCHUNGUZA ONGEZEKO LA SARATANI KANDA YA ZIWA**

SERIKALI imechukua sampuli 700 za watu mbalimbali kuchunguza sababu ya ongezeko la magonjwa ya saratani Kanda ya Ziwa...



UKURASA WA 5

**LE MUTUZ ALIVYOAGWA**

MAMIA ya wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam jana walijitokeza kuuaga mwili wa...

# Majambazi waua watu wanne kikatili, wapora mil. 50/-

UKURASA 3



# Sita watiwa mbaroni tuhuma mauaji daktari, mfanyakazi GGML

• **Mmoja** wa watuhumiwa adaiwa kujinyonga ... *Endelea ukurasa wa 5*

**MICHEZO** NABI ATAJA MBINU KUIMALIZA MARUMO UK.24 **KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongea na wafanyabiashara wa Kariakoo **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgomo Kariakoo ulivyotikisa serikalini

**Na Waandishi Wetu**

SAA 10 za mvutano zilishuhudiwa jana kati ya serikali na wafanyabiashara wa Kariakoo waliogoma kufungua maduka kuanzia asubuhi hadi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipolazimika kuacha shughuli za Bunge jijini Dodoma kwenda Dar es Salaam kuzungumza nao na kuridhia kufungua biashara.

Mapema asubuhi, Nipashe ilitembelea mitaa mbalimbali ya Mkoa wa Kikodi Kariakoo na kukuta maduka yamefungwa huku wafanyabiashara wachache wakiwa katika vibaraza wakijadiliana.

Machinga walikuwa wanaendelea na biashara zao. Wanunuzi wanaochukua bidhaa katika maduka walilazimika kuondoka. Hapakuwa na huduma katika Mitaa ya Swahili, Kongo, Gerezani, Lumumba, Agrey na Sikukuu. Zaidi kulishuhudiwa mabango yenye ujumbe kwa serikali.

Baadhi yalisomeka 'Serikali mtujali wafanyabiashara, tupunguzieni utitiri wa kodi', 'mgomo usio na kikomo mpaka kieleweke', 'usajili wa stoo haukubaliki ni chanzo cha kumfilisi mfanyabiashara', 'imefika mwisho wafanyabiashara tutatuliwe kero zetu', 'Rais ingilia kati Kariakoo inakufa' na 'TRA wametufukuzia wateja wa kigeni'.

Mgomo huo ulidumu kwa saa 10 hadi pale Waziri Mkuu alipozungumza nao na kuwaomba wafungue biashara kwa kuwa serikali imesikia kilio chao na atakuna nao katika kikao maalum kitakachojumuisha mawaziri, maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Bandari (TPA) na viongozi wa wafanyabiashara kujadili tatizo moja hadi lingine na kupata ufumbuzi.

Katika mazungumzo hayo yaliyochukua saa moja, baada ya kumsikiliza Mwenyekiti wa Wafanyabiashara, Francis Mmbwana, Waziri Mkuu aliagiza kusitishwa kwa kikosi kazi hadi serikali itakapotoa utaratibu mwingine.

**ILVYOKUWA**

Kabla ya Majaliwa kwenda Kariakoo, Katibu Mkuu Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Uroki Ombeni, alisema wamefikia hatua hiyo kwa lengo la kupinga usajili mpya ya stoo ambao unamtaka mfanyabiashara kupeleka TRA ripoti ya mzigo uliobaki na uliouzwa.

"Tunapoteza wateja wengi, hapa kuna nchi karibu 12 kutoka nje ya nchi zilikuwa zinakuja kufuata bidhaa, lakini kwa sasa haziji, kuna mambo mengi ambayo Rais akiyafahamu na kuyafanyia kazi taifa litapiga hatua.

"Tunachokihitaji serikali itatue kero, zinazotukabili itushirikishe kwenye vikao vya uamuzi ili na sisi tuchangie mawazo yetu. Wasikae tu peke yao huko wakaamua bila kutusikiliza ili kuepusha matatizo kama haya," alisema.

**WAMGOMEA RC**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, asubuhi alikwenda kuzungumza na wafanyabiashara hao na kuwaeleza kuwa Waziri Mkuu ameomba kukutana nao Dodoma, lakini alipoondoka waliitisha mkutano wao na kutoa msimamo wa kutokwenda Dodoma. Wakaendelea na mgomo.

Walisema wanalipa kodi, hivyo Waziri Mkuu kama anataka kuonana nao, awafuate Kariakoo na siyo wao wamfuate.

**UFAFANUZI TRA**

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi (TRA), Richard Kayombo, akitoa ufafanuzi kwa Nipashe kuhusu suala hilo, alisema kuwa katika kikao chao na wafanyabiashara hao kilichofanyika siku chache zilizopita, walikubaliana wachague viongozi kwa ajili ya kwenda kukutana na Waziri Mkuu Dodoma ili kupatiwa ufumbuzi wa kero zao.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara kusajili stoo zao, Kayombo alisema "...tuliwapa elimu kuhusu sheria inayowataka kusajili stoo za vifaa na magodauni yao kwa kuzingatia sheria iliyopitishwa kwa mwaka wa fedha uliopita.

"Tunalazimika kufanya hivyo kwa sababu baadhi yao wanapuuza sheria hiyo, kwenye magodauni pia tuligundua kuna mchezo mchafu unafanyika kwamba mzigo unaweza kutolewa kwenye godauni kupelekwa kwa mteja kwa risiti moja na ikatumika siku nzima."

**PM KARIAKOO**

Akiwa Kariakoo, saa 10:30 jioni, Waziri Mkuu aliwatakia wafanyabiashara kufungua maduka yao, huku akiahidi kutatua vikwazo vyote walivyoviwasilisha.

Alisema soko hilo linategemewa na nchi nyingi. Siyo Tanzania pekee. Kwa kufanya hivyo kuna hatari ya kuwafukuza wateja wa kutoka nje.

Alikemea kitendo cha baadhi ya maofisa wa TRA kuwaonea baadhi ya wafanyabiashara kwa kuwatolea maneno ya kashifa na kutowasilikiza wanapowasilisha malalamiko yao kwa madai mpaka waone barua rasmi za matamko ya viongozi wa kisiasa.

Kuhusu sheria ya usajili wa stoo ambayo ndiyo sababu kuu ya mgomo huo, Majaliwa aliamuru sheria hiyo kutotumika kwa muda mpaka pale itakapotolewa elimu kwa wafanyabiashara.

"Sheria ya usajili wa stoo ilikuwa na nia njema lakini walikosea kuanza kuitumia bila kutoa elimu, hivyo ninaagiza isitishwe mara moja moja (ili) kuruhusu utoaji wa elimu kuendelea huku wakiangalia namna nzuri ya kulitekeleza hilo," aliagiza.

Waziri Mkuu pia alikemea rushwa kwa baadhi ya maofisa wa TRA. Ni kosa kisheria. Linafanya wafanyabiashara kuendelea kubaki masikini.

"Mbali na rushwa hata kamatakamata haileti sifa nzuri. Mnakamata mpaka wateja wa nje wanaokuja kununua bidhaa, kitendo hicho kitasababisha kufukuza wateja wa kigeni," alionya na kuagiza kufutwa kwa vikosi kazi vilivyoundwa na TRA. Alivitaja ni sababu ya rushwa kati ya wafanyabiashara na serikali.

"Tutwasaidia wafanyabiashara kutatua kero zinazowakabili. Jumatano tutafanya mkutano na viongozi wa wafanyabiashara kwa ajili ya kupokea malalamiko na maoni yao na kuangalia namna ya kuyafanyia ufumbuzi kwa pamoja. Hatokubali Soko la Kariakoo life," aliahidi.

Awali mfanyabiashara wa vifaa vya ujenzi katika Mtaa wa Swahili, Ramadhani Chande alisema uamuzi wa kufanya mgomo umetokana na kutokuridhishwa na utendaji wa TRA. Alisema umejengeka uadui mkubwa kati yao na mamlaka.

Mfanyabiashara wa vifaa vya ujenzi Mtaa wa Gerezani, Suedi Saidi, alisema lengo la mgomo ni kuishinikiza TRA iwajali. Wanaamini njia hiyo itawasaidia kupata haki.

"Ukienda ofisini kwao wanaongea vizuri mno. Ukimkuta Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Kayombo, ana kauli tamu sana lakini kukikucha asubuhi vijana wake hawa hapa. Tumewachoka, hatutaki bugudha."

**VYAMA VYA SIASA**

Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara wa Chama cha ACT-Wazalendo, Halima Nabalang'anya, katika tamko rasmi la chama hicho jana, aliitaka serikali kuchukua hatua za haraka kutatua kero hizo.

Aliitaka serikali kuitazama upya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 kifungu cha 45A kilichopo chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi kinachowataka wamiliki au watumiaji wa maeneo ya kuhifadhi bidhaa, kusajili maeneo hayo kwa Kamishna Mkuu wa TRA.

"Kumekuwa na malalamiko makubwa ya rushwa katika utozaji wa kodi katika eneo la Kariakoo dhidi ya maofisa wa TRA. Hali hii imefukuza wateja wengi kutumia eneo la Kariakoo katika eneo la Maziwa Makuu.

Bungeni jijini Dodoma, Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alisimama kwa kutumia Kanuni ya 54 (1), kuomba kujadiliwa jambo la dharura la mgomo huo wa Kariakoo.

Baada ya hoja hiyo kutolewa, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema lazima ajiridhishe kwanza kabla ya kuruhusu mjadala huo. Akatoa nafasi kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, kutoa ufafanuzi.

Waziri huyo alisema kumekuwa na majadiliano kati ya serikali na wafanyabiashara wa Kariakoo kuhusu hoja zao mbalimbali ambazo wanatamani serikali izifanyie kazi.

***Imeandaliwa na Halfani Chusi (DAR) na Romana Mallya (DODOMA)**

# CCM Zanzibar yampa kongole Rais Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimempongeza Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kukamilisha kwa mafanikio yake ya kichama katika Mkoa wa Mjini.

Katika ziara hiyo Dk. Mwinyi, amekutana na kuzungumza na viongozi wa ngazi za mashina (mabalozi) matawi, wadi, majimbo, wilaya hadi mkoa pamoja na kukagua miradi ya chama na jumuiya zake hatua ambayo ni sehemu ya kiutendaji katika misingi ya kuimarisha chama.

Taarifa iliyotolea na Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Itikadi na Uenezi, imesema kasi ya kiutendaji ya Rais Dk. Mwinyi ni kielelezo tosha cha maendeleo endelevu ya kuifikisha Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi chache za visiwa zilizoendelea kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

Chama Cha Mapinduzi, kinaamini kuwa dhamira, mipango, mikakati na dira za Makamu Mwenyekiti Dk. Mwinyi aliyoitoa katika ziara yake ya kichama katika Mkoa wa Mjini ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi wa CCM ya mwaka 2020/2025.

Dk. Mwinyi, amewahakikishia wana-CCM kuwa ataimarisha miundombinu ya kiuchumi ndani ya CCM ili iwanufaishe wanachama wote.

Pia, CCM Zanzibar itaunga mkono dhamira ya kuthamini juhudi za Rais Mwinyi ya kutekeleza kwa vitendo Ilani ya CCM, ibara ya 136 kifungu kidogo cha (c) kinachoelekeza kuzalisha ajira 300,000 kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi ifikapo mwaka 2025.

# Majambazi waua watu wanne, wapora mil. 50/-

**Na Waandishi Wetu**

MAKUNDI ya watu wanaosadikiwa kuwa ni majambazi yameua watu wanne katika matukio mawili tofauti, mjini Mbozi, Mbeya na Tarime, mkoani Mara, huku katika tukio moja wakivamia kituo cha mafuta, kupora Sh. milioni 50 na kuua watu wawili na huko Tarime wakiua

kwa kuwapiga risasi wakazi wawili.

Katika tukio la Mbozi imeelezwa kuwa watu hao pia walipora bunduki moja yenye namba za usajili CAL 39409 aina ya shotgun ambayo waliitelekeza kando ya reli ya TARAZA katika mji wa Mlowo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, aliwaambia waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Mei 13, mwaka huu majira ya saa saba usiku.

Alisema watu hao ambao hawajakamatwa walivamia kituo hicho wakiwa na silaha za jadi na vifaa vingine vilivyotumika kubomolea chumba maalumu cha kuhifadhia fedha na kuchukua mauzo ya mafuta na simu mbili za wafanyakazi.

"Tunaendelea kuwatafuta watu hao, lakini katika eneo la tukio kulikutwa kisu, bisibisi, pamoja na kifaa cha kuvunjia (tindo), ambavyo vilidodoshwa na majambazi hao," alisema Kamanda Mallya.

Hata hivyo, alisema jeshi hilo linamshikilia mmoja wa walinzi wa kituo hicho, Andoya Mponda (31) kutoka kampuni ya ulinzi ya Bullet Force Security.

Katika tukio la Tarime, watu wawili wameuawa kwa kupigwa risasi katika vijiji vya Nyabisaga na Gwitiryo, Tarafa ya Inchugu, wilayani Tarime mkoani Mara, Ramadhan Musa Keryoba (18) na Otieno Sorai (35) na watu wanaosadikiwa kuwa majambazi.

Kadhalika, wamewajeruhi kwa kuwakata mapanga sehemu mbalimbali za mwili, Moronya Bhoke na

Moraita Gesere, Mei 13, mwaka huu. Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mwenyekiti wa Kijiji cha Gwitiryo, Joseph Timuti na Mwenyekiti Kijiji cha Nyabisaga, Chacha Mohere, walithibitisha kutokea kwa matukio hayo.

Akisimulia tukio hilo, alisema watu hao walivamia na kuteka watu na kisha kuwaua.

"Watu hawa walikuja wamepakizana kwenye pikipiki walimsimamisha Gerese aliyekuwa akirejea nyumbani kwake na kuanza kumshambulia kwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo kichwani, mikononi na mgongoni, alipiga kelele kuomba msaada," alisema.

Alisema kutokana na kelele hizo Moronya na Otieno ambao ni wakazi wa jirani na maeneo hayo, walijitokeza kutoa msaada na walimbeba na kumpakiza kwenye pikipiki, wakati wanafanya hivyo majambazi walijitokeza na kumshambulia Otieno kwa risasi na kumkata kwa panga Moronya.

Alisema baada ya tukio hilo watu hao walikimbilia Kijiji cha Gwitiryo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Gwitiryo, Timuti alisema majambazi hao walimvamia nyumba nyingine wakavunja mlango, familia ilipopiga kelele kuomba msaada, walifyatua risasi kupitia mlangoni na kumpata kichwani Ramadhan Musa, kisha wakakimbia.

Madiwani wa Kata ya Gwitiryo, Nashon Mchuma na Kata ya Pemba, Seronga Wangwe, wamelaani matukio hayo na kuwataka wananchi kuanzisha ulinzi shirikishi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi, Tarime Rorya, ACP Geofrey Sarakikya, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo na kusema wanaendelea na matibabu katika Kituo cha Afya Sirari, huku akiwataka wananchi kutoa taarifa za watu wanaowatilia shaka.

***Imeandikwa na Moses Ng'wat (MBOZI) na Samson Chacha, (TARIME)**



Wafanyabiashara wadogo wakiendelea na shughuli zao pembeni ya mtaro uliojaa maji machafu yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha, Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali: Uraia pacha rukhsa kwa watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imelieleza Bunge kuwa hairuhusu uraia pacha kwa watu wazima isipokuwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Agnesta Lambert.

Alihoji kama serikali iko tayari kuruhusu uraia pacha kwa Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema uraia wa Tanzania unaongozwa na Sheria ya Uraia ya Tanzania Sura ya 357, marejeo ya mwaka 2002.

"Sheria hii inabainisha aina tatu za uraia wa Tanzania ambazo ni uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia wa tajnisi. Kwa mujibu wa Sheria ya Uraia tajwa hapo juu, serikali hairuhusu uraia pacha kwa watu wazima isipokuwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 ambao wanakuwa na uraia wa Tanzania na uraia wa nchi nyingine," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali inapata kigugumizi gani kuleta muswada wa marekebisho wa uraia pacha.

"Katiba ya nchi inakataza ubaguzi wa aina yoyote - kwamba amepata uraia wa nchi nyingine serikali haioni huu nao ni ubaguzi kwao?" Alihoji.

Masauni alijibu kuwa serikali haijajiridhisha kwamba uraia pacha ni matakwa ya wananchi walio wengi na katika mchakato wa Katiba uliokwama, serikali ilipendekeza hadhi maalum kwa kuwa ndiyo matakwa ya wananchi walio wengi.

"Serikali ipo hatua za mwisho kuanza utaratibu wa kuwa na hadhi maalum kwa wanaoishi nje ya nchi na kuna fursa kama 10. Mchakato huu ukikamilika zitatolewa kwa Watanzania waliochukua uraia wa nchi zingine," alisema.

# Serikali kuchunguza ongezeko la saratani Kanda ya Ziwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imechukua sampuli 700 za watu mbalimbali kuchunguza sababu ya ongezeko la magonjwa ya saratani Kanda ya Ziwa.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira.

Mbunge huyo alihoji serikali imefikia wapi kuhusu utafiti wa ongezeko hilo.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema sampuli hizo ziko tayari maabara na zinaendelea kuchambuliwa ili kuona sababu ya kuongezeka kwa magonjwa hayo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, alihoji mpango wa serikali kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa saratani ya kizazi.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema serikali inatekeleza mikakati mbalimbali katika kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa kansa ya kizazi ikiwamo kutoa elimu kwa umma kuhusu kujikinga na ugonjwa wa saratani. Alisema serikali inatoa chanjo (HPV) kwa wasichana ili kuwakinga na kirusi kinachosababisha saratani ya mlango wa kizazi.

"Pia tumeanzisha huduma za awali za uchunguzi na matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za Taifa," alisema.

Dk. Mollel alisema serikali imeimarisha huduma za kibingwa za uchunguzi na matibabu kwa kuhakikisha kuna wataalamu na vifaa tiba kwa ajili ya kukabiliana na saratani.

Katika kujenga maswali ya nyongeza, mbunge huyo alisema Taasisi ya Saratani Ocean Road imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa siku hadi siku hususan wanawake wenye saratani ya kizazi.

"Serikali haioni haja ya kuwasaidia kina mama hawa kufungua vituo vya saratani katika hospitali za kanda na mikoa ili kupunguza gharama za usafiri na mahitaji muhimu? "Kwa kuwa serikali imeonyesha kuna huduma za uchunguzi wa saratani katika maeneo mbalimbali. Je, ina mkakati gani wa kuziunganisha huduma za uchunguzi wa saratani katika kliniki za mama na mtoto ili wapate huduma hiyo?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imejipanga na kwa mwaka huu imetoa zaidi ya Sh. bilioni 200 kwa ajili ya vifaa tiba ambavyo vitasaidia uchunguzi na tiba kwa hospitali za kanda na mikoa.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq, alisema kumekuwapo na waganga wa jadi na wa asili wanadai kutibu saratani na kuhoji kauli ya serikali kutokana na waganga hao ambao wamekuwa wakiwapa taarifa ambazo si sahihi wagonjwa.

Dk. Mollel alisema yeyote atakayeibuka na jambo hilo, wizara imekuwa ikituma wataalamu kutoka kwa Mkemia Mkuu kukiangalia kama ni kweli na ikibainika hakuna tiba anashauriwa kuendelea kufanya utafiti kwa kushirikiana na wizara.




Baadhi ya viongozi wa Daikin Afrika Mashariki na wafanyabiashara wakiwa pamoja kwenye kikao cha wafanyabiashara katika hoteli ya Hyatt Dar es Salaam wikiendi hii. Daikin iliwazawadia wafanyabiashara ambao walifanya vizuri katika vipengele mbali mbali ndani ya mwaka uliopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU: Watoto kukataa kutumwa hadi wapewe kitu ni hatari kwa maadili

**Na Mary Geofrey**

MOJA ya tabia za watoto zinazosababisha mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii ni kukataa kutumwa na watu wazima na kuomba ahadi ya vitu au fedha kwa watu wanaowafahamu na wasiowafahamu.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Joseph Mwaiselo, aliainisha hayo jana wakati akizindua filamu ya Tanjema iliyoandaliwa kwa kuhusisha vikaragosi kwa lengo la kufundisha maadili, haki, kutii sheria na kutimiza wajibu kwa watoto nchini.

Alisema kuanzishwa kwa filamu hiyo kutasaidia watoto kufahamu wajibu na kuutimiza, kutii sheria na kutenda haki kwa wakubwa na wadogo ili kuwa na kizazi kunachozingatia yote.

"Lengo ni kuhakikisha nchi yetu kama ilivyo katika Ibara ya 8 ya Katiba lazima iwe na maendeleo. Lazima kuwe na haki na kama hakuna, maendeleo hayawezi kuwapo ndio sababu filamu hii itasaidia kujenga wanafunzi wetu kuanzia ngazi ya chini," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema rushwa ni uovu ambao unaondolewa na uadilifu, hivyo kupitia filamu hiyo wanafunzi watajifunza maadili mema kwa kuamini kuwa kizazi kijacho kitakuwa salama.

"Waliondaa filamu wanalenga kufundisha umuhimu wa maadili kwa kuzingatia kutimiza wajibu, kutenda haki na kuzitii sheria zilizopo nchini. Mradi huu umefadhiliwa na Ubalozi wa Marekani. Lengo ni kufikisha elimu hii nchi nzima," alisisitiza. Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Wailes, Sameer Khan, alisema wamejifunza kuwa waaminifu, tabia njema, kutimiza wajibu wao na kutenda haki kwa sababu rushwa ni adui wa haki.

"Tumefundishwa kuwa wakarimu, kuheshimu wakubwa na wadogo na tukitumwa na wakubwa tusikatae au kuomba fedha kwanza," alisema Sameer.

# Diwani mwingine afariki kwa ajali

**Na Mary Mosha,** MOSHI

AJALI ya barabarani iliyohusisha lori la mizigo aina ya Mitsubishi Fusso lililogongana uso kwa uso na gari dogo aina ya Toyota Noah, imekatisha uhai wa Diwani wa Old Moshi Magharibi wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro, Menyasumba Macha (55).

Macha anakuwa diwani wa tatu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa kupoteza maisha tangu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, akitanguliwa na Diwani wa Njoro na Kalimawe (Same).

Jana, Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Simon Maigwa, alithibitisha ajali hiyo kugharimu maisha ya diwani huyo.

"Kimsingi, Macha alifikwa na umauti wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC," alisema Maigwa.

Ajali hiyo ilitokea Mei 14, mwaka huu majira ya usiku katika barabara kuu ya Himo/ Moshi, eneo la Kili East Bar katika Kata ya Msaranga. Macha alikuwa anaendesha gari aina ya Toyota Noah lenye namba za usajili T 472 CAM. Alipogongana na Mitsubishi Fusso T 867 AUF.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi, Morris Makoi, alisema kuwa kutokana na kifo hicho, wamelazimika kuahirisha kikao cha robo ya tatu cha Baraza la Madiwani ili kuwapa madiwani nafasi ya kumzika mwenzao.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Mkoa wa Kilimanjaro (ALAT), Swalehe Mkwizu, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mwanga, alisema kuwa Macha alikuwa ni Mjumbe wa Kamati Tendaji ya ALAT Mkoa. Atakumbukwa kwa uongozi wake uliotukuka.

"Majira ya saa 12 asubuhi ya Me 15 nilipokea taarifa za kifo cha mjumbe huyo, ambaye alipata ajali usiku wa Mei 14 katika eneo la Mjohoroni.

"Alikuwa kiongozi machachari. Unapoleta hoja yako katika kikao, ni lazima ujipange vyema. Siyo mtu wa kukubali kila kitu. Hivyo, tumepoteza mtu muhimu kwa ustawi wa maendeleo ya Mkoa wa Klimanjaro," alisema Mkwizu. Wiki iliyopita, mmoja wa madiwani wilayani Songea mkoani Ruvuma alifariki dunia kwa ajali ya pikipiki aliyokuwa anaiendesha.

Katika ajali hiyo, Diwani wa Mtyangimbole katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba mkoani Ruvuma, Erick Herman Mkolo (48), alifariki dunia na watu wengine wawili kujeruhiwa baada ya pikipiki walizokuwa wakiziendesha kugongana uso kwa uso.

# Chongolo aonya wanaojipitisha kwa wananchi udiwani, ubunge

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewatahadharisha wanachama wake wanaoanza kujipitisha kwa wananchi ili kutaka nafasi za ubunge na udiwani waache mara moja kwa kuwa wanakiuka taratibu na miongozo ya chama.

Chongolo aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa ukumbi wa mikutano wa CCM Wilaya ya Bukombe na kuweka jiwe la msingi katika nyumba ya kupumzikia wageni ambao ujenzi wake umefikia asilimia 80 na kugharimu zaidi ya Shilingi milioni 200.

"Niwaambie tu muda bado kwa kufanya hivyo mnakiuka taratibu na kwa kweli tunawaona na tutawachukulia hatua za kinidhamu, chama hiki kina taratibu zake muda wa siasa bado sasa hivi waacheni waliopo wafanye kazi ikifika 2025 nafasi zitatangazwa hapo itakuwa ni ruksa kwa kila mwanachama kugombea ila kwa sasa acheni fitina na uchonganishi," alisema Chongolo.

Aidha, aliwataka watendaji wa halmashauri nchini kusimamia fedha za miradi ya maendeleo zilizopelekwa kwenye halmashauri zao kwa kuwa Serikali ya CCM imetoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha nchi inakua na maendeleo kwa wananchi yanaonekana.

"Nitumie nafasi hii kuwataka watendaji wa halmashauri nchini kuhakikisha mnasimamia kikamilifu fedha zinazoletwa kwenu kwani serikali inadhamiria kuifungua nchi kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana sasa hatutakuwa na muhari wala haya kwa wale watakaochezea fedha hizo, sisi kama chama kinachotawala tunataka kuona wananchi wanapata huduma safi kwa wakati, hivyo hatutakuwa na mchezo na yeyote atakayechezea fedha hizo," alisema Chongolo.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, Wilaya ya Bukombe, Mbunge wa Jimbo la Bukombe na Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alisema Jimbo la Bukombe limetekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ya afya, elimu na miundombinu kwa zaidi ya asilimia 80.

"Katibu Mkuu sisi kwetu kaulimbiu yetu ni kusema na kutenda na kupitia msemo huu tumeweza kushirikiana na kuhakikisha tunakamilisha miradi ya afya, miundombinu na elimu shule za msingi na kata tumeziboresha," alisema Biteko.

Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Saidi Nkumba, alisema mradi huo ulianza Julai 2019 sambamba na ujenzi wa ukumbi wa mikutano mradi huo ulihusisha ununuzi wa samani za ndani ya ofisi na ukumbi, ujenzi wa nyumba ya kupumzikia wageni, ujenzi wa jengo la migahawa, bustani kuzunguka eneo la ofisi ukarabati wa vyoo matundu sita, ujenzi wa uzio, pia ujenzi wa mtandao wa maji na tangi lenye ujazo wa lita 10,000.

Mradi huo umelenga kukinufaisha Chama Cha Mapinduzi wilaya kwa kuwa ukumbi huo utakapokamilika utakuwa chanzo kikuu cha mapato na kukodishwa kwa shughuli mbalimbali wilayani Bukombe.

CCM Bukombe pia inaendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi na itasaidia kupunguza gharama za maisha kwa watumishi na kuongeza ari ya utendaji kazi.

# Polisi yakamata watuhumiwa sita mauaji daktari, mfanyakazi GGML

## ●Mmoja wa watuhumiwa adaiwa kujinyonga

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limewakamata watuhumiwa sita wa mauaji ya Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kerende wilayani Tarime, Dk. Isack Daniel na mfanyakazi wa Mgodi wa GGML, Milembe Seleman.

Mauaji ya Dk. Isack yalitokea Mei 3 mwaka huu saa tatu usiku wakati akitokea kazini kutekeleza majukumu yake. Mfanyakazi wa GGML aliuawa Aprili 26 katika Mtaa wa Matulole mkoani Geita.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo jana, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, alisema watuhumiwa watatu wa mauaji ya Dk. Isack walikamatwa jijini Dar es Salaam. Inadaiwa kuwa baada ya kufanya tukio, walikimbilia Mwanza na baadaye Dar es Salaam.

Misime alisema watu hao wamekamatwa na askari wa jeshi hilo waliobobea katika masuala ya uchunguzi wa matukio ya mauaji na wanatarajia kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kujibu mashtaka yanayowakabili.

"Pamoja na watuhumiwa wa mauaji ya mfanyakazi wa GGML kukamatwa, mtuhumiwa wa nne wa tukio hili amejinyonga baada ya kusikia wenzake wamekamatwa wakiwa na vielelezo walivyotumia katika mauaji hayo pamoja na baadhi ya mali za marehemu."

"Katika uchunguzi wetu kuhusu kisa cha kifo cha Dk. Isack, tumebaini ni wahalifu tu wamefanya uhalifu ili kuiba kama sehemu ya kazi yao," alisema Misime.

Misime alimtaja mtuhumiwa aliyejinyonga ni Pastory Lugodisha, maarufu Buchuchu, ambaye alijinyonga Mei 6, 2023 kwa kutumia mkanda wa suruali katika Pori la Hifadhi ya Buhindi wilayani Sengerema.

"Jeshi la Polisi linatoa tahadhari kwa wahalifu. Waache tabia hiyo na kufanya kazi halali ili kujipatia kipato," alisema Misime.

**MWANAFUNZI UDOM**

Kamanda Misime alisema suala la kifo cha mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Nusura Abdallah, liko katika uchunguzi ambao ukikamilika, watatoa ufafanuzi kwa wananchi. Mwanafunzi huyo aliripotiwa kufariki dunia katika Hospitali ya Faraja, huko Himo mkoani Kilimanjaro.

Kuhusu gari la Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, Misime alisema kanuni, taratibu na sheria zikifuatwa, litatolewa kwa sababu ni mali yake.



Aliyekuwa Waziri Mkuu, John Malecela, akiaga mwili wa mwanawe ambaye ni mmiliki wa Mtandao wa Lemutuz, Wiliam Malecela, katika hafla ya maziko iliyofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Le Mutuz alivyoagwa

**Na Zanura Mollel**

MAMIA ya wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam jana walijitokeza kuuaga mwili wa Mkurugenzi wa Mtandao wa Le Mutuz Tv na blogu maarufu ya Lemutuz Superbrand, William Malecela huku Waziri Mkuu mstaafu ambaye ni baba mzazi wa marehemu, Mzee John Malecela, akisema familia imeyachukua mema yaliyoelezwa na waombolezaji na itayatumia kama nyota katika familia.

Akitoa salamu za shukrani kwa waombolezaji waliofika kuuaga mwili wa mtoto wake katika viwanja vya Karimjee, Malecela alisema familia imefarijika kwa namna watu wanavyomwelezea kijana wao alivyoishi nao vizuri.

"Mambo yote mema yaliyosemwa kuhusu mwanangu, ninaomba familia na ukoo wa Malecela tuyachukue kama nyota itakayotuongoza," alisema.

Rafiki wa karibu wa Le Mutuz, Juma Pinto, alisema William alikuwa wa pekee ambaye akimwambia jambo anaweza kumsikiliza na kulifanya.

Alisema tangu aliporejea nchini toka Marekani, aliendelea na maisha yake na kwamba maisha ya mitandaoni aliyokuwa akiishi "siyo yake halisi".

"Niliwahi kupigiwa simu na watu wawili wenye heshima zao wakidai Le Mutuz anadhalilisha watu kupitia mitandao ya kijamii. Nilimwita na kumshauri kutumia mitandao hiyo kutengeneza marafiki na sio maadui, alinisikiliza. Hata gari la kwanza alilokuwa anatumia William ni mimi nilimnunulia na alikuwa nalo kwa miaka 15 hadi umauti unamkuta.

"Siku moja dada yake ambaye ni marehemu kwa sasa, Dk. Mwele, wakati anajiandaa kuchukua fomu ya kuwania nafasi ya urais kupitia Chama Cha Mapinduzi, aliniita na kunieleza kuwa anakwenda kuchukua fomu ya kugombea urais ila hakutaka William kumposti kwenye mitandao yake ya kijamii kwa sababu tayari ana watu wake.

"Nilimwitikia kisha nikamweleza William. Baada ya kumweleza, alifunga safari kuelekea Dodoma na kwenda kumsaidia dada yake katika hatua hiyo, baadaye Dk. Mwele alinipigia simu kunishukuru sana, Willium alikuwa ana roho nzuri sana," alisema Pinto.

Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaha, alitoa pole kwa kipindi hiki kigumu kwa familia ya Malecela. Rais Samia Suluhu Hassan ametoa ndege kwa ajili ya kusafirisha mwili hadi Dodoma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jamii Forums, Maxence Melo, alisema amefahamiana na Le Mutuz kwa zaidi ya miaka 20 na wameshirikiana kwa mengi na alimtambua kama sauti ya umeme, na miongoni mwa wanachama wachache walioanzisha mtandao huo, ikiwa ni sehemu ya kuchochea maendeleo nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Klabu ya Yanga, Haji Manara, alisema urafiki wao ulianzia baada ya Le Mutuz kurejea nchini kutoka Marekani na kwamba sifa yake kuu ilikuwa ni kutunza muda na hapendi kugombana.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jukumu la kulea familia lisiachwe upande mmoja

**WAKATI** jana ikiwa Siku ya Familia, jamii inakumbushwa kuwa jukumu la kulea familia linahusu pande zote.

Mke na mume wanapoamua kuanzisha familia, wote kwa pamoja wanapaswa kupanga jinsi ya kulea familia yao kwa kushirikiana.

Hatahivyo, katika miaka ya hivi karibuni kuwa na tabia ya wanandoa kuachiana mzigo wa kulea watoto kuanzia chakula, mavazi mpaka ada za shule. Mara nyingi hukumu hilo huachiwa mwanamke na kubebeshwa mzigo mkubwa wa kulea familia.

Tabia hiyo imeelezwa kuwa ni chanzo kimojawapo cha watoto kukosa maadili mema katika jamii.

Mama au baba anapoelemewa na majukumu wakati mwingine hushindwa kufuatilia mienendo ya watoto wao.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokuwa katika maadhimisho ya Siku ya Mama Duniani, jijini Dar es Salaam juzi, ambayo yalienda sambamba na uzinduzi wa taasisi ya Binti Lindi Initiative, alisema ni muhimu wazazi waangalie na kufuatilia kwa karibu mienendo ya watoto wao ikiwamo tabia zao na maendeleo yao shuleni na kuwa karibu na walimu.

Aliwasihi kinababa kuacha kukimbia majukumu na malezi kwa watoto wao na kuwaachia wanawake peke yao kwa kuwa kufanya hivyo kunachangia kwa asilimia kubwa mmomonyoko wa maadili na vitendo vya ukatili kwa watoto.

"Niwaombe wanaume wenzangu chondechonde suala la maadili linaelekea pabaya watoto wetu wanaharibika, jahazi linazama, hivyo tuondokane na kuwaachia wake zetu malezi, tunakabiliwa na tatizo la mmomonyoko, tubadilike."

Kauli hiyo ya Waziri Mkuu inakumbusha jinsi sasa hivi maadili yalivyoporomoka ya watoto kuharibika na kujiingiza katika utamaduni ambao hapo zamani haukuwapo nchini.

Kutofuatiliwa kimalezi, watoto wanaingia katika wimbi la kuiga maisha ya mitandao yanayoonyesha watu kumiliki majumba ya kifahari au kuwa na magari mazuri bila kufikiri kuwa wakati mwingine hayo ni maisha ya maigizo.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Khamisi, akizungumzia hali hiyo, alisema tayari wameshaunda madawati maalumu ya watoto katika shule za msingi na sekondari ili waweze kuripoti vikwazo vinavyowakabili watoto wanapokuwa huko.

Wengine huogopa kuwasiliana na wazazi wao kwa hofu ya kupigwa au kutishiwa na watu wanaowafanyia vitendo hivyo.

Alisema watoto wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo vingi vya kimalezi huku wakiwa hawana pa kusemea, na kwamba wizara imeona ianzishe madawati hayo, ili kuwafikia kirahisi.

"Wazazi kwa pamoja tushirikiane katika malezi, ili kupata jamii bora, kwani jukumu la malezi ni letu sote, asiwepo wa kukimbia majukumu na kumwachia mwingine."

Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Lindi, Kijakazi Yunus, katika kupigia msumari suala hilo anakumbusha kuwa malezi ni jukumu la watu wote kuanzia ngazi ya familia, jamii hadi taifa na kwamba kwa ushirikiano huo ni rahisi tukatengeneza taifa bora.

Jamii ione umuhimu wa kuangalia watoto bila kujali umemzaa wewe. Tukumbuke wazee wetu walivyokuwa wakiwalea watoto hata kama sio wa kwake akiona amekwenda kinyume na maadili atamkanya na kumripoti kwa mzazi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Ilivyo nyepesi, ngumu rasimu sera ya elimu

**WIZARA** ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imekuja na rasimu ya sera ya elimu toleo la mwaka 2023 ambayo imejadiliwa na wadau wa sekta hiyo na wataalamu kwa kutoa maoni mbalimbali yenye lengo la kuiboresha.

Binafsi naipongeza wizara kwa uamuzi wa kuboresha mfumo wa elimu, ambao utakwenda sambamba na mabadiliko yaliyopo katika dunia ya sasa kwa kuzalisha Watanzania watakaokuwa na utaalamu.

Utekelezaji wa mtaala mpya na sera ya elimu ya mwaka 2023 utaanza kwa awamu, kwa darasa mojamoja katika kila ngazi, kwa kuwa serikali imeweka wazi kwamba hatua hiyo itafanikishwa kwa kwenda sawia na bajeti, ikimaanishwa utekelezaji unafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha za kugharamia masuala yote yanayokuja na rasimu.

Lakini pamoja na hayo, nina hoja kidogo kuhusu uamuzi kwamba miaka minne ya sekondari haitakuwa ya hiari tena tofauti na sera iliyopo ambayo inasema elimu ya lazima ni kwa shule za msingi pekee. Kwa ujio huo elimu ya sekondari sasa ni lazima na haikwepeki.

Ninadhani mfumo huo ungeendelea kwa elimu ya msingi kuwa ya lazima badala kuuweka kwenye elimu ya sekondari, kutokana na ukweli kwamba kiwango hicho cha elimu mwanafunzi anafikia kulingana na uwezo wake wa darasani hasa kuanzia la kwanza hadi la saba.

Kama itakuwa ya lazima kwa maana ya mwanafunzi kupata ujuzi wa fani fulani ya kumsaidia maishani, itakuwa sawa, lakini kama ni kutaka avuke vidato bila kuwa na uwezo darasani, anaweza kukimbia.

Mbali na hapo, ninakubaliana na hatua zinazochuliwa na wizara ili kuboresha kwa nia ya kuwaandaa vijana waweze kujitegemea baada ya kuhitimu kidato cha nne badala ya kubaki wakirandaranda mitaani.

Lakini inaelezwa kuwa kufanya kwa madarasa yote na ngazi zote ni gharama kubwa, hivyo kwa ngazi mojamoja, utekelezaji ukitarajiwa kuanza mwaka 2024 baada ya sera na mtaala vitapitishwa kama ilivyo.

> **Ninaamini Kiingereza kikiendelea kuwa kama somo, bado wanafunzi watakuwa na shida katika lugha hiyo ya kigeni, hasa wanapoanza kidato cha kwanza na kukutana nayo.**

Wakati kukiwa na mkakati huo, ninadhini ni vyema mafunzo yakaanza kutolewa, kwa ajili ya wale watakaotekelezaji wa mtaala huo wakiwamo walimu na wadau wengine ili kuendana na mabadiliko hayo.

Vilevile, si vibaya wafanyakazi wangeongezwa, ili waendane na mahitaji ya utekelezaji wa mtaala ikiwamo walimu wa kozi na masomo mapya, kwa maana kwamba serikali ijiandae kwa bajeti ya kutosha.

Hapa ninamaanisha kwamba kuwe na fedha za kutosha kugharamia miundombinu mbalimbali katika maeneo ya kutolea elimu, lakini mishahara ya uhakika na vitabu vya kutosha.

Pamoja na hayo, ni vyema uwepo mwongozo kwa wanafunzi watakaochukua mkondo wa amali, ili wajue ni fani zipi zinaendana na vipaji vyao, malengo yao, uwezo wao na hata uhitaji katika soko la ajira.

Aidha, kulingana na maendeleo ya dunia kwa sasa, uamuzi wa Kiingereza kufundishwa kuanzia darasa la kwanza kwa shule za Kiswahili na Kiswahili kitafundishwa kuanzia darasa la kwanza kwa shule za Kiingereza, ni hatua nzuri na kupongezwa.

Ninaamini Kiingereza kikiendelea kuwa kama somo, bado wanafunzi watakuwa na shida katika lugha hiyo ya kigeni, hasa wanapoanza kidato cha kwanza na kukutana nayo.

Hivyo, ninadhani sasa wanafunzi wa shule za umma nao wanaweza kuondokana na mtihani huo wa kutojua lugha ya Kiingereza wamekuwa wakikumbana nao kila wanapoanza kidato cha kwanza.

Lakini taifa lipende lisipende Kiingereza ndiyo lugha ya kiteknolojia, kielektroniki na ndiyo inayobeba mawasiliano ya sekta na nyanja zote duniani hivyo inahitaji kupata uzito maalumu na siyo ya kukwepwa tena.

HABARI KITAIFA

## Majaliwa: Kinababa washiriki malezi watoto kujenga maadili

**Na Pilly Kigome**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka jamii ishirikiane na kinamama katika malezi ili kujenga jamii yenye maadili ya kitanzania.

Alitoa wito huo juzi usiku alipozungumza na washiriki wa hafla ya Mtoko wa Mama katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam. Alishiriki maadhimisho ya Siku ya Mama Duniani katika hafla iliyoandaliwa na Taasisi ya Binti Lindi Initiative.

Kinababa washirikiane na kinamama katika malezi ya watoto kwani kidole kimoja hakivunji chawa. Sote tumelelewa na kinamama zaidi, lakini kinababa tunapaswa vilevile kujipa muda na kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto kuanzia asubuhi mpaka usiku," alisema.

Waziri Mkuu alitoa wito kwa jamii kuheshimu na kuthamini mchango wa mama katika malezi, akisema "…kama wahenga walivyosema, 'kuzaa siyo kazi ila kazi ni kulea mwana'. Tushirikiane na kinamama wote katika malezi ili kwa pamoja tujenge jamii yenye maadili ya kitanzania.

"Ninatambua kuwa mama zetu katika karne hii mnafanya shughuli nyingi za kiuchumi kwa ajili ya ustawi wa familia na taifa kwa ujumla. Niwasihi sana mwendelee kuwa vinara katika suala la malezi ya watoto," alisisitiza.

Aliwataka wazazi na walezi kutambua kuwa wao ni taasisi muhimu na ya kwanza katika malezi ya mtoto. Alisema: "Timizeni wajibu wenu, shirikianeni na taasisi za kiserikali ili kukuza na kuimarisha maadili kwa watoto wenu pamoja na kutenga muda wa kuwafuatilia ili kujua changamoto zao na kuwelea ipasavyo."

Akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na washiriki wa hafla hiyo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamisi, alisema Siku ya Mama Duniani huadhimishwa kila Jumapili ya pili ya mwezi Mei.

Alisema kumekuwa na matukio mbalimbali ya ukatili kwa watoto na wizara yake iliamua kuunda madawati ya watoto katika shule zote za msingi na sekondari ili wapate mahali pa kujieleza pindi wakiona dalili ama wakifanyiwa ukatili.

"Hadi kufikia Machi 2023, madawati 1,488 yameundwa ambapo 1,070 yako katika shule za msingi na 418 yako sekondari. Lengo letu ni kuzifikia shule 25,000 nchini," alisema.

Sophia Mbeyele, mwalimu wa Shule ya Sekondari Makumbusho mkoani Dar es Salaam, alisema katika hafla hiyo "…lishe isipokuwa kamili kwa mtoto, inaweza kuleta ulemavu hata kama alizaliwa akiwa mzima (bila ulemavu)."

Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Lindi Initiative, Kija Yunus, alisema "…niwasihi vijana tuwaheshimu wazazi wetu na kamwe tusiwaone kuwa wamepitwa na wakati kwani sikio halizidi kichwa. Tuepuke vishawishi vya fedha vinavyoweza kuwa chanzo cha kuleta tatizo la kimaadili miongoni mwetu."



Wafanyakazi wakiendelea na kazi katika nyumba ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme wa Julius Nyerere, wakati wa ziara ya wajumbe wa kamati ya usimamizi wa mradi huo ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi husika mkoani Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Singida yaundiwa mkakati kuwa kitovu cha biashara

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema ujenzi wa barabara za lami unaoendelea na utakaoanza hivi karibuni, una lengo la kuufanya Mkoa wa Singida kuwa kiunganishi na kitovu cha biashara kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Kati, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini.

Akizungumza juzi mjini Itigi katika hafla ya utiaji saini mikataba ya ujenzi wa barabara zinazoingiliana katika Daraja la Sibiti zenye urefu wa Km 24.83 na barabara ya Makongolosi-Rungwa-Itigi-Mkiwa, sehemu ya Noranga hadi Doroto (Km 6) na Itigi hadi Mkiwa (Km 25.569) kwa kiwango cha lami, Prof. Mbarawa aliwataka wakazi wa Mkoa wa Singida kujipanga kutumia fursa za miradi hiyo kujikwamua kiuchumi.

"Ujenzi wa kipande cha Noranga - Doroto na Itigi - Mkiwa ni mwendelezo wa juhudi za serikali kuifungua barabara yote ya Makongorosi-Rungwa-Itigi hadi Mkiwa kwa kiwango cha lami, na hivyo kuiunganisha mikoa ya Singida na Mbeya kwa urahisi zaidi," alisema Prof. Mbarawa.

Waziri huyo aliwataka viongozi wa Mkoa wa Singida kuwapa ushirikiano wa kutosha mkandarasi China Henan International Cooperation Group Co. Ltd. (CHICO) na wataalamu wengine wanaojenga barabara hizo ili zikamilike katika ubora uliokusudiwa na mapema zaidi.

"Viongozi wa Mkoa na wa TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania), hakikisheni vijana wa Mkoa wa Singida wanapata kipaumbele katika kupata ajira kwenye miradi inayoendelea ili kuwawezesha kunufaika kwa kupata utaalamu na kukua kiuchumi," aliagiza Prof. Mbarawa.

Barabara hizo zitakapokamilika, zitaunganisha kirahisi mikoa ya Singida, Simiyu, Shinyanga, Arusha, Dodoma na Tabora na kufanya Mkoa wa Singida kunufaika na shughuli za kilimo, utalii na biashara.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Rogatus Mativila, alisema kuwa barabara zinazoingia katika Daraja la Sibiti zitakapokamilika, zitaondoa adha ya usafiri katika daraja hilo na hivyo kuvutia wasafirishaji wengi kupita njia hiyo.

Mativila alisema kuwa ujenzi huo utahusisha upanuzi wa makaravati makubwa na madogo na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika sehemu zenye mmomonyoko wa udongo.


Mbunge wa Manyoni Magharibi, Yahaya Masare, akizungumza kwa niaba ya wabunge wa Mkoa wa Singida, aliishukuru serikali kwa namna inavyotekeleza miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara mkoani hapa.

Barabara ya Itigi hadi Mkiwa ni sehemu ya barabara itokayo Mbeya kupitia Makongorosi-Rungwa-Itigi hadi Mkiwa yenye urefu wa Km 413 ambapo sehemu ya Mbeya-Lwanjilo hadi Chunya (Km 72) na Chunya - Mkongorosi (Km 39) tayari imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Katika hatua nyingine, Prof. Mbarawa amesema tayari serikali imeshapata mkandarasi atakayejenga barabara ya Handeni-Kibirashi hadi Singida (Km 462) na maandalizi ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Arusha-Kongwa Junction (Km 438), Mbulu-Hydom (Km 400) na Ifakara-Lupilo-Malinyi hadi Namtumbo (Km 480) yatakamilika mwezi ujao.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# TMDA yaimarisha mfumo kudhibiti uingizaji dawa

**Na Devota Mwachang'a**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imesema imeimarisha mifumo ya usimamizi katika kudhibiti uingizaji wa dawa duni nchini kwa lengo la kuhakikisha ubora na usalama kwa afya ya mtumiaji.

Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Dawa za Binadamu na Mifugo wa TMDA, alitoa kauli hiyo wakati wa mkutano ulioandaliwa na mamlaka hiyo na kuwakutanisha wadau wa uagizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa nchini, kujadili changamoto zinazohusiana na uingizwaji na usajili wa dawa, zikiwamo za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi -VVU (ARV).

Dk. Yonah Mwalwisi alisema "... uchunguzi wa maabara unaonyesha kiwango cha kuwapo dawa duni nchini hakizidi asilimia tano kwa mwaka. Hii ni hali nzuri kwa nchi. Serikali imefanya jitihada kubwa katika kusimamia wafanyabiashara wa dawa kwa ujumla."

Dk. Mwalwisi alisema TMDA inapokea malalamiko yasiyozidi wastani wa kati ya 10 na 15 kwa mwaka toka kwa wateja dhidi ya kuwapo dawa duni sokoni. Yapo malalamiko yaliyotolewa baada ya mteja kuhisi kuwa mwonekano wa dawa umebadilika kulinganisha na aliyokuwa anaitumia awali.

"Jukumu letu ni kumwelimisha mwananchi kuwa tayari tumepokea maombi ya mtengenezaji wa dawa hiyo ya kubadilisha mwonekano ila ubora wake ni uleule. Ni jukumu letu kuhakikisha mtumiaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi anapata bidhaa bora na salama," alisema.

Dk. Mwalwisi alibainisha wataendelea kuchunguza na kubaini mtandao unaohusisha uingizaji, usambazaji na uzalishaji wa dawa bandia, ili kusitisha biashara hiyo haramu inayotishia afya za wananchi.

"Kuna hatua nyingi tunazochukua dhidi ya wanaojihusisha na biashara ya dawa bandia. Kwa wale waliokamatwa hivi karibuni taratibu za kisheria zinaendelea kuchukulia dhidi yao na masuala ya upelelezi yanaendelea," alisema.

Mkurugenzi wa Dawa za Binadamu na Mifugo wa TMDA, Emmanuel Alphonce, alisema waingizaji wengi wa dawa ndiyo wanaouza dawa hizo, hivyo wanapaswa kufahamu masharti ya kuzingatia na kuafuata utaratibu katika kutekeleza majukumu yao.

"Matokeo ya kikao hiki yatakwenda kurahisisha mchakato wa kushughulikia changamoto zilizopo, ili vibali vitolewe kwa wakati kwa lengo la kuongeza upatikanaji dawa salama, bora na zenye ufanisi kwa watumiaji," alifafanua.

Mfamasia kutoka Laborex Tanzania Ltd, Geoffrey Yambayamba, alipongeza TMDA kuboresha mifumo iliyowezesha kutatua changamoto za usajili.

"Uboreshwaji wa mfumo huo ni jambo muhimu na lenye maana kwa jamii kwa kuwa umeturahishia na kuongeza kasi katika usajili na ufanisi, hivyo dawa zitapatikana hospitalini na kuwafikia wagonjwa kwa wakati," alisema Yambayamba.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, akizungumza katika mkutano wa kuhamasisha jamii kuepuka rushwa ya ngoni, Tabata Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' inayoendeshwa na shirika hilo kupitia ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wananchi 10,000 wafikiwa mradi wa maji wa mamilioni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ZAIDI ya wakazi 10,000 wa Kata ya Kauzeni, Manispaa ya Morogoro, wameanza kunufaika na mradi wa maji baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kupeleka huduma iliyogharimu Sh. 592,192,422.94.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Morogoro, Grace Lyimo, alisema MORUWASA ilianza kutekeleza mradi huo Januari na utakamilika Julai 16, mwaka huu.

Alisema uwezo wa mradi ni kutoa huduma kwa watu 10,550. Kwa sasa umeanza kutoa huduma kwa watu 5,512. Lyimo alisema gharama za mradi huo zinahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji katika Mto Tangeni (banio), ujenzi wa kusambaza mabomba ya maji na kusafirisha maji, ujenzi wa tangi kubwa la lita 300,000 na ujenzi wa mabomba ya kusambazia maji kwa jamii.

Alisema mpaka sasa mkandarasi ameshalipwa Sh. 359,344,647.40. Anadai Sh. 144,954,622 ambazo wako katika hatua ya kulipa. Alisema faida ya mradi ni kupata huduma ya majisafi na salama na yanayotosheleza, huku wakiinua uchumi wa wananchi wa Kauzieni kwa kuokoa muda mwingi wanaotumia kutafuta maji, wakiacha shughuli zao za kiuchumi.

Alisema mradi huo pia utasaidia wananchi kuondokana na magonjwa yanayotokana na ukosefu wa maji safi na kuondoa adha ya mama na watoto kuhangaika kutafuta maji.

Alisema mradi huo umeboresha huduma ya maji katika kaya 200, taasisi tatu ambazo ni Shule ya Msingi Kauzeni, Shule ya Sekondari Kauzeni na Zahanati ya Kauzeni.

Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Tamim Katakweba, aliitaka jamii kuhamasika kuingiza maji nyumbani kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizowekwa.

Alisema MORUWASA kwa sasa inaendelea kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na kupanda miti, ili kufanya huduma ya maji iwe endelevu.

Kabla ya kuzindua mradi huo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Abdala Shaib Kaim, alisema huduma ya maji ni muhimu kwa jamii, hivyo mradi huo unapaswa kutunzwa ili uwe endelevu.

## Vodacom yajivunia faida nono mapato ya huduma

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Mawasiliano ya Simu ya Vodacom Tanzania imetangaza ripoti ya awali ya miezi 12 iliyopita inayoishia Machi 31 mwaka huu, ikionyesha ukuaji mkubwa kwa kuzalisha Sh. trilioni 1.1 za mapato ya huduma.

Akizungumza na wawekezaji na wadau wengine wa kampuni hiyo juzi kwa njia ya mtandao wakati wa kutangaza matokeo ya awali ya ripoti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, alisema ripoti imeonyesha kuimarika kwa faida kwa mwaka uliopita. Kumechochewa na kampuni kutimiza adhma yake ya kutoa huduma kwa wateja na shughuli mbalimbali za kunufaisha jamii ya Watanzania nchini.

"Ni fahari kwamba tumepiga hatua kwa mwaka uliopita huku tukiwa tumetekeleza adhma ya kutoa huduma kwa wateja wetu kadri ya mikakati tuliyojiwekea. Imetutia moyo kuona namna tulivyofanikisha miradi mbalimbali ya shughuli za kijamii na kujiendesha kwa faida.

"Vodacom imeonyesha kupata faida ya Sh. bilioni 44.6 baada ya kodi. Ni hatua kubwa kulinganisha na hasara ya Sh. bilioni 20.3 kwa mwaka uliopita. Ukuaji huu umechochewa na ongezeko la matumizi ya intaneti, kuimarika kwa M-Pesa, ongezeko la ukuaji katika pato la kudumu, ambalo ni ongezeko mara mbili kwa mwaka, na kuzalisha faida ya kuridhisha katika mapato ya huduma," alisema.

Alifanunua kuwa mapato ya kupiga simu yamepungua kwa asilimia 1.2 na kufikia Sh. bilioni 283.5 kutokana na ushindani mkubwa wa bei. Mapato ya M-Pesa yamekua kwa asilimia 8.4 na kufikia Sh. bilioni 357.1 kutokana na matumizi ya huduma mpya.

Mkurugenzi huyo alibainisha mapato ya matumizi ya intaneti yameongezeka kwa asilimia 34.2 na kufikia Sh. bilioni 273.7. Kuna uhitaji mkubwa wa matumizi ya huduma za intaneti na ukuaji wa simu janja.

"Ukuaji wa pato la kudumu umeongezeka kwa asilimia 27.3 na kufikia Sh. bilioni 19.5. Kumetokana na uwekezaji katika miundombinu na ongezeko la wateja wapya," alieleza.

Kwa mujibu wa Philip, mapato kabla ya riba, kodi, kushuka kwa thamani na upunguzaji wa madeni yameongezeka kwa asilimia 9.7 na kufikia Sh. bilioni 329.4. Kumechochewa na ukuaji wa kiasi kikubwa na ufanisi katika kudhibiti matumizi. Alisema kampuni imeonyesha ufanisi licha ya changamoto mbalimbali za kiuendeshaji zinazoendelea duniani.


Alisisitiza Vodacom Tanzania imepiga hatua katika utekelezaji wa miradi ya kijamii. Inatumia fursa ya teknolojia kuboresha maisha na maendeleo.

"Tumeongeza usajili wa wakulima katika huduma yetu ya M-Kulima na kufikia milioni 3.1 kutoka 140,000 ambao walisajiliwa mwezi Machi 2022. Kupitia M-Pesa, jumla ya Sh. bilioni 4.6 ziligawanywa kwa wakulima ambao walijiunga, kutoa usalama na ufanisi wa miamala ya kifedha, taarifa za masoko na utabiri wa hali ya hewa," alisema.

Philip pia alisema kampuni hiyo ilijikita katika mpango wake wa ujumuishi katika kujali, uliolenga kuwezesha mazingira rafiki ya kutoa huduma kwa watu wenye mahitaji maalum.

Alisema madawati maalum ya kutolea huduma katika maduka yalianzishwa na kutekeleza huduma ya kutumia lugha ya alama kwa njia ya video katika mtandao wa kijamii wa WhatsApp. Zaidi ya wateja 1,300 walinufaika kutokana na mpango huo kwa mwaka uliopita wa fedha.

Philip pia alikumbusha kuwa mwaka 2022, Vodacom Tanzania ilizindua mtandao wa huduma ya 5G kwa mara ya kwanza nchini, ikiwa ni utekelezaji wa dhamira ya kampuni ya kuipeleka Tanzania katika zama za kidigitali kupitia mikakati endelevu.





# Madiwani waitaka TARURA kukarabati barabara

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MADIWANI wa Halmashauri ya Arusha iliyoko Wilaya ya Arumeru, wameelekeza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kufanya ukarabati wa dharura kwenye miundombinu ya barabara zilizoharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha wilayani humo.

Walitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TARURA katika Wilaya ya Arumeru kwa kipindi cha robo ya tatu ya Januari hadi Machi, mwaka huu.

Akiwasilisha azimio la baraza hilo katika mkutano wa baraza hilo, Diwani wa Olmotonyi, David Kinisi, alisema licha ya serikali kutengeneza barabara hizo, mvua iliyonyesha imesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara, huku akiitaka TARURA kuweka mipango mkakati wa kufanya ukarabati ili ziweze kupitika na kuwaondolea adha wananchi wa maeneo hayo.

"Licha ya kwamba Halmashauri ya Arusha, kwa kushirikiana na TARURA kuchukua hatua za awali za kuzibua mitaro na kuweka vivuko vya dharura, pia tunaiomba serikali kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa namna ya kupata suluhisho la kudumu la kuzuia maji yatokanayo na mafuriko ya maji ya mvua yasilete madhara kipindi cha mvua,"alisema Joseph Tinayo, Diwani wa Olturumet.

Akijibu ombi hilo, Kaimu Meneja wa TARURA, Wilaya ya Arumeru, Mohamed Bakari, alisema tayari ofisi yake imeainisha mtandao wa barabara zilizoharibika na kuziwasilisha Serikali Kuu kupitia ofisi ya waziri mwenye dhamana, kwa ajili ya kuomba fedha za dharura, kipindi cha msimu wa mvua utakapopita ziweze kutumika kufanya matengenezo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Seleman Msumi, alitaja maeneo yaliyoathirika zaidi na mvua na kuharibu miundombinu ya barabara kuwa ni kata za Oloirien, Olturumet, Olmotonyi, Kimnyaki na Sambasha.

"Waheshimiwa madiwani, baada ya serikali kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika na mafuriko yaliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha sehemu mbalimbali za wilaya ni kata za Oloirien, Olturumet, Olmotonyi, Kimnyaki na Sambasha.

"Tunaendelea na mpango wa kuzibua mitaro ya kupitisha maji na kujenga miundombinu iliyoharibika," alisema.

# Serikali yavutiwa maonyesho ubunifu, vipaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imevutiwa na maonyesho ya ubunifu, vipaji na stadi za wanafunzi yaliyoanzishwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), miaka 11 iliyopita na kuagiza menejimenti ya chuo hicho kutengeneza na kuwasilisha wizarani ripoti ya kitaalamu inayoonyesha tathmini nzima ya mafanikio ya wahitimu wake kuchangamkia fursa za ajira sekta binafsi na kuajiri.

Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Utafiti na Maendeleo (Sayansi) wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Ladislaus Mnyone, ameagiza jana kuandaliwa kwa ripoti hiyo ili serikali ivisukume vyuo na taasisi nyingine za elimu ya juu kujifunza kwenye ubunifu huo, wakati ambao taifa liko kwenye mchakato wa kuhuisha sera ya elimu na mafunzo pamoja na mitaala ya elimu.

Prof. Mnyone, alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. James Mdoe, katika tukio la fani, ubunifu na vipaji kwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, yaliyofanyika Mei 11 na 12, mwaka huu.

"Tubadilishe fursa ziweze kutusaidia mtu mmoja mmoja, na kwa ajili ya kutengeneza ajira kwa wengine. Mkiendelea hivi kutumia fursa mtafika mbali sana. Na kutokana na umuhimu huu, niuombe uongozi wa chuo mtengeneze taarifa ya tathmini ya miaka yenu 11 ya utaratibu huu ili tuweze kuona vyuo vingine au taasisi nyingine za elimu ya juu, zinaweza zikajifunza nini kwenye hiki ambacho ninyi mmeweza kukifanya.

"Naamini kuna mengi ya kujifunza MoCU, iwe kwa mtu binafsi au kundi la watu wengi, hasa katika masuala ya ajira na kujiajiri wenyewe. Kwanini nimekumbuka kulisema hili, ni kwa sababu kama inavyonekana serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imo kwenye mchakato wa kuhuisha sera yetu ya elimu na mafunzo lakini vilevile na mitaala ya elimu.

"Mwelekeo ni kuhakikisha sekta yetu na Wizara ya elimu inaenda sahihi katika kuwafanya vijana wawe na ujuzi, lakini mwisho wa siku uwe na uwezo wa kutenda na kufanya vitu ambavyo vinasaidia ule mchakato wa mabadiliko. MoCU bila shaka inaweza ikawa ni mfano mzuri sana wa kuigwa katika ubunifu, sera yetu na mitaala ambayo inahuishwa.

"Ni imani yangu kwamba moja kati ya matatizo yanayolikabili taifa letu ni kuongezeka kwa idadi ya vijana wanaohitimu masomo yao mwaka hadi mwaka. Ukiangalia ule uwiano, kati ya wanaohitimu na ajira zilizoko haviendani kabisa. Ndiyo maana maadhimisho kama haya chuo chetu wameanzisha, yatatusaidia kuhakikisha vijana wanaotoka hapa sio tu wanaweza kuajirika, lakini wanaweza wakajiajiri na wakaajiri wengine."

Kabla ya agizo hilo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (Taaluma), Prof. John Safari, alisema kwa kuwa suala la ajira limekuwa tatizo kwa wahitimu wengi nchini, serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa wahitimu wa vyuo kutafuta fursa mbalimbali ziliko katika mazingira yao ya kujiajiri na wanapoweza waajiri pia na vijana wengine.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Annà Shinini (katikati), ambaye ni Mwenyekiti wa Shirika lisilo la kiserikali la Nasaru akizungumza na wanawake wa Kata ya Emboreet kuhusu mikakati ya maendeleo na uwezeshaji juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Amwomba DC kutumia mamlaka kunusuru vyanzo vya maji Hai

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Edmund Rutaraka, 'amemwangukia' Mkuu wa Wilaya hiyo, Amir Mkalipa, akimwomba kutumia mamlaka yake, kuvinusuru vyanzo vitano vya maji ambavyo ni tegemezi, vilivyovamiwa na wananchi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi, huku baadhi yao wakivitumia vibaya kwa kupuliza sumu za mbolea za viuatilifu kwenye mazao waliyolima ndani ya mita 60.

Rutaraka, alilazimika kuomba nguvu hiyo ya Mkuu wa wilaya, baada ya kamati ndogo aliyoiunda Machi 11, mwaka huu kuchunguza uharibifu wa mazingira, kuwasilisha ripoti yake katika kikao cha robo ya tatu ya mwaka kwenye Baraza la Madiwani la wilaya hiyo.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), tunakuomba kwa nafasi yako utusaidie kudhibiti hali hii katika maeneo yanayotajwa kukithiri kwa uharibifu wa mazingira, hasa kama hili la upuliziaji wa sumu za mbolea za viuatilifu unaoendelea ndani ya mto na vyanzo vingine vya maji pamoja na shughuli za upikaji wa pombe haramu ya gongo unaoendelea ndani ya mto haukubaliki.

"Kamati imeeleza kwa kina kwamba kuna miti mingi imeng'olewa na miti mingine wananchi wanaikausha kwa dawa. Yale yanayotuhusu sisi, namwelekeza Mkurugenzi (DED), awabane wenyeviti wa serikali za vijiji, watendaji wa vijiji na kata na achukue hatua kwa wakuu wa shule waliotajwa kuhusika katika uharibifu wa mazingira."


Awali, akiwasilisha ripoti ya uchunguzi ya kamati hiyo, Mwenyekiti wake Nassib Mndeme, ambaye ni Diwani wa Mnadani (CCM), alisema Mto Kware, wananchi wamelima mpaka kwenye chanzo cha maji. Wakati katika Bonde la Hifadhi ya Mto Kinamiri, wananchi wanaolima wameng'oa miti mingi imeng'olewa na wanaikausha kwa dawa licha ya kuwa chanzo hicho ni muhimu kwa ustawi na kilimo cha umwagiliaji na viumbe hai, ndani ya Kata ya Weruweru na Kata ya Masama Rundugai na mradi wa majisafi wa Makalama.

Kamati yake inapendekeza wananchi hao waondolewe ndani ya eneo hilo na ufanyike utaratibu wa kuotesha upya miti kama ilivyokuwa awali. Aidha, wananchi wasiruhusiwe kujimilikisha tena kuyatunza mazingira kama awali, kwa kuwa ndiyo chanzo cha kukausha chanzo hicho cha Mto Kinamiri.

"Ni vyema maeneo hayo yakabaki chini ya uangalizi wa serikali za vijiji na Halmashauri ya Wilaya na Bonde la Pangani. Lakini pia Bonde la Mto Weruweru, tumekuta mtu mmoja amejenga ukuta ndani ya mita 60 za Mto Weruweru. Pia ameweka bicon (alama za mipaka) ndani ya eneo la mto, tunapendekeza mtu huyo abomoe ukuta na kuondoa alama za mipaka alizoweka na kuotesha miti ya asili 200 katika eneo lote alilojenga ukuta.

"Na katika chemichem za Mto Kiladeda, pande zote zimeharibiwa kwa kukatwa miti, kilimo kinachoendelea ndani ya mita 60 za ulimaji wa mboga aina ya saladi zilizooteshwa ndani ya chemchem na kusababisha baadhi kukauka," alisema.

Mndeme alisema hali ni mbaya zaidi katika Bwawa la Boloti, ambako kuna uharibifu mkubwa unaotokana na shughuli za binadamu, kama kuchoma moto, kukata miti na kulima ndani ya bonde la bwawa.



# TANESCO Simiyu yaomba radhi kukatika umeme

**Na Alex Sayi,** MASWA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Simiyu limeomba radhi kwa wakazi na watumiaji wa huduma ya umeme mkoani humo kutokana na hali ya kukatika kwa umeme ambayo imekuwa ikijitokeza mara kadhaa na kueleza kuwa hali hiyo imekuwa ikisababishwa na hitilafu katika transfoma.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Ofisa Uhusiano wa shirika hilo mkoani Simiyu, Jimmy Jeremia, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kufuatia kadhia hiyo ambayo imekuwa ikitokea mara kadhaa hali inayosababisha hasara kwa watumiaji wa huduma hiyo. "Kiukweli kama shirika tunakiri kuwapo kwa kero hii na hatufurahi kuona ikitokea, lakini umeme wetu tunaupokea kutoka Ibadakuli unasafiri umbali wa kilomita 95 na mtandao wake kwa Maswa ni zaidi ya kilomita 580 na unaendelea kuongezeka tunazo transfoma 292 hivyo wakati mwingine inakuwa ngumu kubaini chanzo cha tatizo lilipo hali inayotubidi kufanya ukaguzi kwa kila transifoma," alisema Jeremia.

Aliongeza kuwa shirika hilo linamatumaini makubwa juu ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa umeme unaoendelea kwa sasa mkoani humo utakaogharimu Sh. bilioni 48 unaotarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18 utasaidia kupunguza kero hiyo kwa kufunga kituo kikubwa cha kupoza umeme Imalilo Bariadi.

Ofisa Usalama Tanesco mkoa, Japhet Lufano, alitoa wito kwa wateja wa shirika hilo kujenga tabia ya kuvilinda vifaa vyao vinavyotumia umeme kwa kuweka vipoza umeme majumbani na ofisini, kufunga mfumo wa umeme 'wiring' kwa kutumia mafundi waliosajiliwa na kununua nyaya na vifaa vyenye ubora.

Meneja Tanesco Wilaya ya Maswa, Mhandisi Issack Fimbo, aliomba radhi kwa hitilafu ambazo zinajitokeza wilayani humo na kubainisha kuwa shirika hilo linaendelea kutandaza nguzo za zege kwenye maeneo korofi ili kupunguza tatizo hilo.

Awali, wananchi mkoani humo walikuwa wakilalamikia uongozi wa shirika hilo kutokana na kero ya katika kwa umeme hali inayosababisha uharibifu wa vifaa majumbani.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi hao walionesha kukerwa na katizo hilo la umeme bila taarifa hali inayowapa shaka ya utendaji kazi wa shirika hilo huku wakiingia hasara ya vifaa kutokana na kuungua mara kadhaa.



Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga, Hamisi Majogolo, akizungumza na wakulima wa zao la tumbaku Kata ya Uyogo, Halmashauri ya Ushetu na kuwakumbusha namna ya kupanga madaraja, kutochanganya tumbaku safi na chafu ili kuepuka kuchafua masoko. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Walalamika kukosekana huduma ya choo soko kuu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wa Soko Kuu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia soko hilo kukosa huduma ya choo kwa muda mrefu licha ya kulipia ushuru katika halmashauri hali inayowalazimu kutumia kilichoko katika kituo kikuu cha mabasi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walisema licha ya soko hilo kukosa huduma hiyo, vilevile meza zimeharibika na mifumo mibovu ya majitaka inayotishia kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko.

Agnes Willison, mfanyabiashara sokoni hapo alisema, licha ya kulipa ushuru wa bidhaa mara mbili watokapo katika minada na waingiapo sokoni, halmashauri imeshindwa kuwajengea miundombinu ya choo ili kudhibiti milipuko ya magonjwa mbalimbali.

"Meza zimechakaa na hakuna vyoo kwa ajili yetu wafanyabiashara na wateja, lakini kwenye makazi yetu endapo kaya ikiwa haina choo inafungiwa na kutozwa faini hili ni tofauti katika soko letu hili," alisema Agnes.

Mwenyekiti wa soko hilo, Athuman Shukia, alithibitisha soko hilo kukosa huduma hizo muhimu na kuahidi kusimamia kila mfanyabiashara katika soko hilo analipia ushuru wa meza, vizimba, taka na bidhaa na kuwataka viongozi husussani Ofisa Biashara kutatua matatizo hayo.

Akijibu malalamiko hayo, Ofisa Masoko wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Chalya Kipindula alisema, utaratibu wa kukusanya ushuru unafanyika kila soko hata kama mtu amelipia ushuru soko aliponunulia bidhaa anapopeleka soko lingine kufanyiabiashara anapwaswa kulipia kisheria.

Kuhusu huduma ya choo na miundombinu mingine, Kipindula aliwataka wafanyabiashara kwa kushirikiana na uongozi wa soko kuandika barua kwa kuanisha mahitaji yao muhimu ya sokoni hapo na kuiwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Anderson Msumba kwa ajili ya kuandaliwa bajeti na kuwawekea mazingira mazuri ya kibiashara.

# Wachimbaji kuanzisha benki yao

**Na Waandishi Wetu**

WACHIMBAJI nchini wamekuja na wazo la kuanzisha benki yao ambayo itawasaidia katika shughuli zao mbalimbali za uchimbaji madini ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa masharti nafuu na kuepukana na mikopo umiza kutoka taasisi mbalimbali za ukopeshaji.

Wazo hilo lilitolewa katika kilele cha mkutano mkuu na kongamano la madini lililofanyika kitaifa mkoani Mwanza huku serikali ikiombwa kuweka baraka katika wazo hilo na kuruhusu kuanzishwa ili kupunguza kero za wachimbaji nchini.

"Tukitengeneza benki yetu na mimi kampuni yangu itakuwa tayari kuchangia mtaji wa milioni 200 mpaka milioni 500 kwa sababu nina uchungu kwa yale nimeyapitia mimi na sipendi na wenzangu wayapitie katika kutafuta mafanikio na wizara ikiweka baraka zake katika hili utakuwa mwanzo wa mafanikio," alisema Baraka Ezekiel, mjumbe wa FEMATA na mmiliki wa kampuni ya Busolwa Mining ya Geita.

John Bina, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini Tanzania (FEMATA), aliunga mkono hoja hiyo na kutumia mwanya huo kuelezea changamoto zinazowatesa wachimbaji wadogo hasa ikilinganishwa na utitiri wa kodi na tozo mbalimbali.

Katika hatua nyingine wachimbaji wadogo wa dhahabu mkoani Geita, walisema wanakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa vya uchimbaji madini pamoja na kutoaminiwa kwenye taasisi za kifedha na kusababisha shughuli za uchimbaji kuwa ngumu.

Kilio hicho kilitolewa na Katibu wa Chama cha Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Geita (GEREMA), Golden Hainga, wakati wa hafla ya ufunguzi wa ofisi mpya ya kampuni ya uuzaji wa vifaa vya kisasa vya uchimbaji madini na mitambo GF Trucks Equipment, soko kuu la dhahabu mkoani humo.

Alisema kuwa uchimbaji madini kwa kutumia dhana duni unachangia wachimbaji wengi kupata uzalishaji mdogo wa madini huku wakitumia gharama kubwa kuendesha shughuli za uchimbaji wa madini.

Aidha, Mkurugenzi wa biashara na masoko wa kampuni hiyo, Salman Karmali, alisema wameamua kuingia ubia na taasisi za kifedha ili kuwasaidia mikopo ya vifaa vya kisasa na mitambo, wachimbaji wadogo na wa kati ili kufanikisha shughuli zao.

Aliwataka wachimbaji wadogo wa madini mkoani humo pamoja na mikoa jirani kuunda vikundi vya wachimbaji vitakavyo wawezesha kukopesheka.



Ukurasa 14

Enzi mpya Vitambulisho vya Taifa usajili ulipokwenda kielektroniki



Ukurasa 13

Mila na desturi ni tiba mpya ya kuhifadhi viumbe, mazingira Afrika

Nipashe
TESA
Jumanne Mei 16, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

**Fahamu unachofanya kubadili kifungo gerezani kiwe cha nje**

ELIMU

EDNA MGUNDA NA PANKRAS LUOGA

# Msondo kufunza watoto, mabinti unyumba anguko la elimu Tunduru

INASHANGAZA lakini ni ukweli kuwa leo karne ya 21 kuna wazazi na walezi wanaowafundisha mabinti zao wadogo hata wale wa miaka minane, masuala ya faraghani, wakiwafunda na kuwaelimisha kwa bidii namna ya kuishi na mwanamume.

Ndiyo msondo, mafunzo ya 'jando' kwa wavulana na 'unyago' kwa mabinti wenye chini ya miaka 14, yanayoendeshwa na Wayao wilayani Tunduru kwa lengo la kumwandaa mtoto kwa maisha ya unyumba na utu uzima bila kujali kuwa wamewahi mno kumpa shule hiyo inayompeleka gizani badala ya kumwangazia mwanga.

Wanachofunzwa ni namna na msisitizo zaidi kwa watoto wa kike kuishi vizuri na mwanaume katika maisha ya ndoa, wakielekezwa na watu wazima na hapa walengwa ni wasichana wenye miaka 14. Lakini, cha ajabu hata watoto wa umri wa chini ya miaka nane nao hushiriki katika mafunzo ya kimila ya msondo.

Wanapewa darasa hilo wakati ambao walitakiwa kuwa shuleni, jambo linalowakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu ili kujiandaa na maisha yao ya baadaye.



Mila na desturi zinazowafunza wasichana maisha ya unyumba na ukeketaji hukwamisha juhudi za kuendeleza elimu. **PICHA: MTANDAO**

### LENGO NI NINI?

Mafunzo haya yanadaiwa kuwa na umuhimu mkubwa katika jamii hiyo huko Tunduru kwani lengo ni kutumika kumwonyesha msichana au mtoto wa kike kuwa tayari amekua, ana majukumu, hadhi na heshima iko juu na pia ana thamani kubwa mbele ya wanajamii wenzake.

Kiujumla mafunzo haya yaliwekwa kwa lengo zuri ila yamekuwa yakitumika vibaya kwa kutojali umri wa watoto na nini wanachotakiwa kujifunza kwa wakati huo.

Nipashe ikueleze kwa ufupi maana, athari za kielimu zitokanazo na mafunzo ya msondo yasiyo sahihi kulingana na umri wa watoto wa kike hasa waliopo shuleni wilayani Tunduru na nini kifanyike kumkomboa.

Msimamizi wa mradi wa "Kijana Jiongeze" wilayani Tunduru, mkoa wa Ruvuma Edna Mgunda, kutoka shirika linalohusika na masuala ya ushauri wa kiafya na lishe COUNSENUTH, anasema kumekuwa na matumizi yasiyo sahihi ya mafunzo kwa watoto wa kike hivyo kuwakwamisha kielimu.

Ni jambo linalogundulika wakati wa utekelezaji wa mradi wa Kijana Jiongeze wenye lengo la kuongeza ufaulu na uwezo wa wanafunzi wengi hasa wa kike ili kujiunga kidato cha tano na kuendelea, kujiamini na kujithamini na kupata stadi za maisha ili kuajiriwa au kujiajiri baada ya kumaliza masomo.

Hata hivyo, inaonekana kuwa mafunzo hayo kwa sasa yamelenga zaidi katika kuwaandaa zaidi watoto wa kike kwa maisha ya utu uzima hasa ya kuishi na mwanaume bila kujali kuwa ni kuchochea ndoa na mimba za utotoni.

### KINACHOJIRI

Edna anasema baada ya mafunzo hayo ya kimila msichana huanza kuitwa "mama" hivyo kuwa na maamuzi kamili bila kuingiliwa na wazazi au wanajamii wengine, kuamua kuhusu masomo yake kwa maana ya kwenda shule au la, kuendelea na masomo au kuacha kusoma muda wa kurudi nyumbani, kulala nyumbani au kwenda popote pamoja na kuwa na marafiki wa kike au kiume.

Hata hivyo, ameeleza kuwa kwa jamii ya Tunduru watoto wengi huanza kupatiwa mafunzo hayo mapema hata kabla ya kufikisha umri wa miaka nane. Kwa maana hiyo watoto wa umri huu bado ni wadogo na hutakiwa kuwa shuleni.

Na mbaya zaidi mafunzo haya yamekuwa yanafanyika kipindi cha masomo.

### KITAKACHOTOKEA

Nini kinatokea kwa mwanafunzi wa kike wakishapatiwa mafunzo haya? Edna anajibu akisema kuwa iwapo mwanafunzi wa kati ya miaka 8 na 14 anayesoma kuanza kufahamu masuala ya mapenzi tena kwa undani, husababisha wasiwe na malengo wala sababu ya kupata elimu na kuanza kufikiria zaidi kujihusisha na ngono na mahusiano.

Hata hivyo, Edna anasema lilikuwa ni tatizo kubwa lenye madhara kwenye maendeleo ya kielimu ya mtoto wa kike hasa kabla ya kuanza kwa mradi huo na sasa katika utekelezaji wa mradi wa Kijana Jiongeze unaotekelezwa wilayani hapo kwa miaka miwili sasa.

Mafunzo hayo huwafanya watoto wengi wa kike kuanza kujisikia kuwa tayari wamekua wakubwa, wapo huru na kuweza kuamua mambo yao wenyewe ikiwa ni pamoja na masuala ya mahusiano ya kimapenzi na kuwa na wapenzi bila kuulizwa wala kufuatiliwa na wazazi na walezi, hata kama wanaishi pamoja.

Zaidi, anasema hali hii huwafanya wanafunzi hawa wa kike

INAENDELEA UK.13

ELIMU
NA JAMES LAUREAN

# Fahamu unachofanya kubadili kifungo gerezani kiwe cha nje

KIFUNGO ni adhabu mshtakiwa apewayo baada ya kupatikana na hatia kwenye makosa ya jinai kutokana na jambo alilofanya halikubaliki kwenye jamii, mfano ujambazi, mauaji, wizi na ubakaji, baada ya hapo huwa mfungwa.

Kifungo hakipo kwenye kesi za dawa au madai na kama kitatumika kuna utofauti kidogo katika mwenendo wa adhabu hiyo.

Adhabu, mahakamani zipo za aina kadhaa mfano kifungo cha jela kinachomaanisha kutumikia adhabu gerezani. Kinaweza kuwa kifungo cha kipindi fulani baada ya kukutwa na hatia.

Kinachotolewa kulingana na sheria iliyovunjwa au kukiukwa na pia kwa mujibu wa uzito wa ushahidi uliotolewa mahakamani katika kuthibitisha mashtaka pasipo shaka.

Aidha, katika kifungo hicho kinachotokana na utetezi wa mshtakiwa, au utashi wa jaji au hakimu kwa mfano kupigana au kumpiga mwenzako, hukumu yake haiwezi kuwa sawa na ujambazi.

Kadhalika kuna hukumu ya kifungo cha nje cha moja kwa moja kutoka kwa hakimu au jaji, kinachompa mamlaka kumhukumu mshtakiwa aliyekutwa na hatia adhabu hiyo ndani muda fulani kulingana na makosa aliyofanya.

Kuna pia kuhukumiwa kulipa faini kwa mlalamikaji au serikali au vyote kwa pamoja. Katika hukumu hiyo mahakama huamuru mshtakiwa aliyekutwa na hatia kulipa faini kwa mlalamikaji ya kiasi fulani cha pesa kama fidia lakini inaweza kumtoza faini kuilipa serikali kama adhabu ndogo.

Suluhu ya kifungo hiki ni kutafuta pesa zilizohitajika kulipwa mahakamani na baada ya hapo mshtakiwa aliyekutwa na hatia kuachiwa huru baada ya malipo.

Kifungo hiki hutumika kwa watu ambao wamepigana hadharani, kutukanana na kudhalilishana, shambulio la kudhuru mwili na kusababisha madhara kwa mlalamikaji.

Ipo hukumu nyingine ya kifungo gerezani, kipo cha nje na faini au vyote vitatu kwa pamoja na mshtakiwa huamuriwa vyote kutokana na kosa alilolifanya.

Hapa mshtakiwa anatakiwa kulipa faini na kutumikia adhabu gerezani kwa pamoja, kushindwa kulipa faini kunaweza kusababisha aliyekutwa na hatia kuongezewa muda wa kifungo zaidi.



Baadhi ya wafungwa wakishona nguo za aina mbalimbali. Katika kurekebisha tabia wanaweza kutumikia adhabu ndani au nje ya gereza. **PICHA: TPS BLOG**

> Suluhu ya kifungo hiki ni kutafuta pesa zilizohitajika kulipwa mahakamani na baada ya hapo mshtakiwa aliyekutwa na hatia kuachiwa huru baada ya malipo.

### UNAWEZA KUOMBA KIFUNGO

Ikumbukwe kuwa unaweza kumuombea mfungwa aliyekutwa na hatia kifungo cha nje hata kama kahukumiwa kutumikia adhabu gerezani.

Ikiwa ndugu au rafiki amehukumiwa baada ya utetezi akaangukia katika hukumu namba moja ya kutupwa gerezani na kifungo chake hakijazidi miaka mitatu, unaweza kumwombea kifungo cha nje, kwa mujibu wa kifungu na 3(2) (a) cha Sheria ya Huduma kwa Jamii ya mwaka 2002.

Kifungo cha nje ni utaratibu ambao unampa fursa mfungwa kutumikia kifungo chake nje ya gereza kwa kufanya shughuli au kazi zisizo na malipo kwa manufaa ya jamii.

Baada ya hukumu, mfungwa atakwenda gerezani na kutumikia kwa muda kisha ataomba kupitia kwa Mkuu wa Gereza , au mkuu wa gereza huyo kwa kuangalia na kutathmini mwenendo wa tabia zake atamshauri mfungwa kutumikia kifungo cha nje na kuwasilisha nyaraka za maombi katika mahakama ili kushughulikiwa.

Sheria ya Magereza Sura ya 58 kifungu namba 52 (1) (2) inatoa utaratibu wa kumwondoa mfungwa aliyepo gerezani mwenye sifa ya kutumikia kifungo kwa utaratibu wa huduma kwa jamii.

Aidha, mahakama inaweza kutoa hukumu ya kifungo cha nje moja kwa moja mahakamani kwa mshtakiwa au mfungwa.

### MAHUDHURIO NJE

Kifungo cha nje kinatumikiwa katika kuhudumia ofisi mbalimbali za mahakama au taasisi za umma, mfungwa hutakiwa kufika saa 12 asubuhi mahali alipopangiwa kuripoti kwa ajili ya adhabu yake na kumaliza saa 4 asubuhi.

Mfungwa anayetumikia kifungo cha nje ni lazima aishi kwa kufuata sheria na masharti aliyopangiwa, ieleweke kuwa anakuwa chini ya uangalizi maalumu, kama kutoondoka nje ya mkoa bila kibali na kuhakikisha kuwa hatendi kosa la kijinai mpaka muda wake wa kifungo utakapokamilika.

Aidha, anaonywa kutojiingiza katika makosa ya kijinai na kama hatafuata masharti anaweza kusababisha kurudishwa gerezani na kukosa haki ya kutumikia kifungo hiki cha nje.

### FAIDA KIFUNGO NJE

Zipo nazo ni pamoja na kupata muda wa kuwa na familia, kuwa na uhuru na familia, mfungwa anaweza kuwaona wapendwa wake, mke wake na watoto na kushiriki katika malezi ya watoto tofauti na anapokua gerezani.

Hii ni fursa inayowasaidia wengi sana na kuimarisha ustawi wa jamii na mfungwa wakati anatumikia adhabu yake na kujutia makosa yake anapata pia nafasi ya kuona familia muda wote.

Jingine ni kufurahia uhuru mchache unaopewa, akiruhusiwa kutembelea maeneo yoyote ndani ya mkoa wake, kutembelea wapendwa wake kuhudhuria sherehe au misiba kitu ambacho gerezani hawezi kukipata.

Ni unafuu kwa mfungwa mwenye matatizo kiafya, huwasaidia kuwaimarisha na kusaidia afya zao kuliko wakiwa gerezani.

Hupata nafasi ya kufanya kazi, kujiajiri au kuajiriwa, aidha kifungo cha nje humwezesha mfungwa kupata kazi kwa kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe na kutunza familia yake na wanaomtegemea.

Hili pia limewasaidia wafungwa wengi katika kuimarisha uchumi wao, kujifunza na kuacha uhalifu, kutafuta kipato kwa njia halali na kuheshimu sheria.

Baadhi ya wafungwa huwa walimu na kuzingatia sheria za nchi, lakini pia kifungo kinamgeuza mfungwa balozi mtaani na mtu anayezingatia sheria.

Wafungwa wengi wamebadilika maisha yao na wengine kuwafundisha wenzao huko kwenye jamii namna ya kuondokana na uhalifu na kuacha matendo mabaya.

### CHANGAMOTO

Japo kifungo cha nje kinaweza kuwa ni neema kwa mfungwa, ni shubiri katika kuitelekeza. Kuna changamoto nyingi wanazokutana nazo wafungwa katika kutumikia huduma hizi za kijamii.

Nazo ni pamoja na muda wa kuondoka ambao sio rafiki kwa wafungwa kufanya kazi, kufika eneo la huduma saa 12 asubuhi na muda wa kuondoka ni saa 4 asubuhi, wafungwa hawa hufanya kazi kwa kushirikiana na hivyo humaliza kazi zao mapema kabla ya muda wa mahakama kuanza.

Kazi mahakamani huanza saa 2:30 asubuhi, wafungwa wanakua wamemaliza kazi lakini hulazimika kusubiri mpaka saa 4.00 ili kusaini na kuondoka kulingana na masharti ya kifungo.

Hili huwa changamoto hasa katika maeneo ya miji hasa Dar es Salaam, wafungwa hawa saa nne wanayotoka wanashindwa kutafuta kazi na kama wanapata kazi wanashindwa kuifanya kutokana na kutoka mida ambayo ni mibaya, kwa Dar es Salaam usafiri unatakiwa kukadiria walau saa nzima kufika safari yako hilo linafanya mfungwa anaruhusiwa aendako atafika saa 5:00, hakuna mwajiri atakayekubali uingie kazini saa 5:00 pengine kwa utaratibu mwingine.

ELIMU

NA JENIFER GILLA, BRAZZAVILLE

# Mila na desturi ni tiba mpya ya kuhifadhi viumbe, mazingira Afrika

MATUMIZI ya mila na desturi za wananchi wazawa wa sehemu zenye misitu asilia barani Afrika yamedhihirika kuwa ni mkakati unaofaa kutunza bayoanuai zilizopo ndani ya misitu inayowazunguka kwenye kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Ni maelezo ya wanawake wazava wanaosema kuzingatia mila na desturi zao ni njia kuu wanayoitumia kutunza viumbe hai kuanzia wanyama, wadudu, mimea na viumbe wengine kwenye maeneo yao ya Afrika ya Kati na Bonde la Kongo.

Wanayasema hayo kwenye Kongamano la Kwanza la Wanawake Wazawa wa Afrika ya Kati na Bonde la Kongo linalofanyika Brazzaville, nchini Jamhuri ya Congo linaloandaliwa na mashirika ya REPALEAC na Right Resources Initiative (RRI).

Baadhi ya mila hizo ni kukataza kula kila nyama inayopatikana katika misitu yao pia kuingia bila kibali kutoka kwa viongozi wa kimila kwa kuwa inaaminika misitu hiyo hulindwa na mizimu, aidha kuficha aina za miti dawa wanayoitumia kuepusha wageni kuivamia na kuimaliza.

Kadhalika, wanataja mila nyingine ni kuwachukulia wanyama kama ni ndugu na marafiki wao hivyo wanapopita katika maeneo yao hawawagusi pamoja na kufunga shughuli za kuvua na kuchota maji kwenye mito kwa muda huku wakiamini kuwa inalindwa na mizimu.

Mariam Gisero kutoka mkoani Mara, akizungumzia ulinzi wa misitu kwa kutumia mila na desturi zinazohusisha wanawake, anaiambia Nipashe kuwa anatoka kwenye msitu wa Mibango Butiama, akisema wanaamini kuwa msitu huo unalindwa na mizimu ya mababu zao hivyo yeyote haruhusiwi kukata miti bila kibali kutoka kwao.



Jamii za watu asilia wataalamu wa fani mbalimbali za jadi wakishiriki kongamano jijini Brazzaville. **PICHA: JENIFFER GILLA**

"Inaaminika kuwa yeyote atakayekwenda kinyume ataiudhi mizimu ambayo hugeuka wanyama wakali na kumdhuru. Imani hiyo imechangia kuhifadhi bioanuai iliyopo katika misitu hiyo."

Kutoka Kenya, Teresa Chemosop kutoka jamii ya Waogiek, analiambia Kongamano la Kwanza la Wanawake Wazawa wa Afrika kuwa, anapotoka hairuhusiwi kuua tembo kwa sababu anaaminika kuwa ni ndugu wa wanadamu na atakayefanya kosa hilo anaachiwa laana na ukoo ambayo humfanya kuwa kichaa au kupotea hapo kijijini.

"Sisi tembo ni ndugu yetu wa damu, atakayebainika amemuua anapelekwa kwenye baraza na kuonywa na yeye anaapa kuwa hatorudia na ikitokea kuwa amerudia analaaniwa na ukoo na kutoweka ," anasema.

Kiongozi wa jamii za wazawa kutoka kijiji cha Bananing nchini DRC, Kabile Angel, anasema katika kijiji chake wanawake hawaruhusiwi kula nyama ya chui kwa kuwa inaaminika atakayekula anaaibisha mila hivyo atapata madhara ikiwamo kuugua.

Anasema pia si kila mwanamke anaruhusiwa kwenda kuchimba dawa msituni, bali kuna watu maalum wenye utaalamu wa namna ya kuchuma dawa hizo na hiyo inafanyika ili kuepuka uharibifu wa miti inayotoa dawa hizo na taarifa zake kufahamika kwa jamii za nje na mbali ambazo zinaweza kuiharibu.

"Kuna namna maalum ya kuchuma dawa, kwa sababu kuna miti ukiikata vibaya inakufa, kwa hiyo kuna watu wenye utaalam na kuzijua dawa hizo kikamilifu ndiyo wanaokwenda kuchuma, yoyote atakayekwenda kinyume na masharti haya anaadhibiwa," anasema.

Naye Ndumeimana Gracia kutoka Burundi, anaeleza kuwa katika jamii yake huwa wanafunga mto kwa muda kuwa hakuna mwanamke anayeruhusiwa kuchota maji au kuvua samaki katika kipindi hicho na atakayekiuka kama hataombewa msamaha kwa mizimu atapata madhara.

Mkurugenzi wa Mikakati wa Shirika la kiraia la Christensen Fund la Marekani, Casey Box , linalotoa msaada wa kifedha kwa wazawa ili kulinda rasilimali zao anasema mila na desturi zina nafasi kubwa ya kuhifadhi mazingira kwa wazawa wa jamii zenye mizitu barani Afrika.

Anaeleza kuwa mfuko wa Christensen Fund, unawekeza kuimarisha uhusiano kati ya mazingira asilia na tamaduni za wanadamu na kwamba hutoa ruzuku zinazokuza manufaa ya ulinzi jumuishi wa kibaolojia, kiikolojia na kitamaduni katika maeneo mbalimbali duniani ikiwamo Congo.

Anasema kwa uzoefu aliokuwa nao wa kufanyakazi na wazawa wa jamii zilizozungukwa na misitu kwa miaka 10 amegundua licha ya juhudi kubwa wanazofanya wazawa ya kuhifadhi bioanuai wana changamoto ya kutokuwa na usalama wa maisha yao baada ya kuibuka tabia ya serikali kuwaondoa kwenye maeneo yao.

"Nafikiri hakuna haja ya kuwaondoa wazawa hawa, serikali inapaswa ikae nao chini kuangalia njia bora wanaweza kufanya ili waendelee kuwapo bila kuathiri shughuli ya uhifadhi, hili jambo linawezekana kwa sababu tumeona baadhi ya maeneo jamii zinaishi na wanyamapori bila tatizo lolote," alisema.

Mratibu kutoka Shirika la RRI la Marekani, Solange Bandiaky-Badji, anazishauri serikali kushirikiana na jamii hizo ili ziendelee kutunza rasilimali kupitia imani zao ili jamii nzima ikiwamo taifa inufaike na uwapo wake.

"Shirika letu limekuwa likisaidia wanawake wazawa walioko katika jamii zilizozungukwa na misitu kwa sababu tunaelewa nguvu waliokuwa nayo katika kuzihifadhi, lengo ni kuhakikisha wanaendelea kutumia mila na desturi zao kulinda na kuhifadhi rasilimali hizo muhimu," anasema.

## Msondo kufunza watoto, mabinti unyumba anguko la elimu

**INATOKA UK.11**

ambao wapo shule za msingi na sekondari kutumia mafunzo hayo kuanza mahusiano tena na wavualana wanaosoma nao, hawajali kuhudhuria masomo, hawafanyi vizuri darasani, kuacha shule bila kuulizwa na wazazi, walezi au wanajamii.

Mbaya zaidi huamua kubaki wengine huolewa mapema huku wakikatisha ndoto zao za kielimu. Anakumbusha kuwa wengi wao ni watoto ambao wana chini ya miaka 14 , miili na akili zao bado hazijawa imara na kuwa na uwezo wa kuhimili maisha ya ndoa. Hivyo suala hili linawafanya baadhi ya wanajamii hao ambao walitakiwa kuwa wanafunzi katika shule mbalimbali kushindwa kufikia ndoto zao za kielimu na kupata madhara ya kiafya pia.

### MADHARA KWA WASICHANA

Kulingana na maelezo ya msimamizi wa mradi Edna, ni pamoja na watoto wa kike kujifunza zaidi mambo ambayo si muhimu katika maisha yao kwa sasa. Mfano mtoto wa kike wa miaka sita au nane kujifunza jinsi ya kuishi na mwanaume wakati hajapevuka hupelekea kufikiria mambo ya mapenzi na wanaume kuliko masomo.

Na mwisho hufanya watoto kuanza kuona kuwa elimu si kitu cha msingi sana katika maisha yao bali mahusiano ya kimapenzi na kuishi na wanaume ni kipaumbele. Mbaya zaidi hali hii huanza kuathiri maendeleo yao ya kielimu, kiafya, jamii, uchumi na maendeleo ya vijiji vyao.

Anatoa mfano kuwa baada ya mafunzo ya msondo wanafunzi wengi wa kike wamekuwa wakianza kujihusisha na masuala ya mapenzi na watoto wenzao shuleni, mitaani, walimu na pia wanajamii wengine japo bado shuleni.

Wengine wanaamua kuacha shule, kuolewa wakiwa katika umri mdogo tena bila kuwa na ujuzi wala stadi za maisha na uwezo wa kujitegemea kijamii na kiuchumi.

### UFUMBUZI

Edna anasema kwanza jamii lazima itambue kuwa mafunzo ya msondo kwa watoto si jambo mbaya ila wajali umri na mahitaji yao ya muda mfano kama ni kusoma waachwe wamalize shule, pili, matumizi na mafunzo sahihi ya msondo inatakiwa iangaliwe vizuri na isitumike vibaya ili kuwafanya watoto wa kike kuanza kujifunza mambo ya ndoa na jinsi ya kuishi na mwanaume.

TEKNOLOJIA

NA ROMANA MALLYA

# Enzi mpya Vitambulisho vya Taifa usajili ulipokwenda kielektroniki

MSONGAMANO wa watu katika Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) karibu saa nane,

kuanzia saa 1:30 asubuhi, muda ambao hutumika kwa uzalishaji mali, umeifanya mamlaka hiyo kuboresha huduma zake kwa kujikita zaidi kujiendesha kidigitali.

Katika kuboresha huduma zake za utoaji wa vitambulisho vya taifa, mamlaka hiyo imeamua kutengeneza mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (online registration), ili kuondokana na changamoto hiyo.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano NIDA, Godfrey Tengeneza, anabainisha kwamba, tangu waanze huduma ya utoaji vitambulisho vilivyozalishwa ni 11,423,829 ambapo kati ya hivyo, vitambulisho 9,703,222 vimegawiwa kwa wananchi husika.

Anaweka wazi kwamba mfumo mpya wa usajili kidigitali lengo lake si kuongeza kasi ya uzalishaji wa

vitambulisho, isipokuwa unarahisisha mchakato wa usajili kwa kupunguza muda mrefu ambao mwananchi anautumia akienda kusajili katika ofisi za usajili wilayani.

Tengeneza anasema katika eneo la usajili na utambuzi wa watu, kumekuwa na ongezeko kubwa la wananchi wanaohitaji huduma hiyo.



Vitambulisho vya Taifa. **PICHA: NIDA**

"Hali hii inasababisha msongamano wa watu wengi katika ofisi zetu za usajili wilayani. Kwa kuzingatia hilo, tumeamua kutengeneza Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao yaani (Online Registration), ili mwombaji aweze kusajiliwa katika mfumo wa vitambulisho vya taifa, ni lazima afike katika Ofisi ya NIDA (wilaya) anayoishi kupata huduma.

Anaeleza kuwa usajili wa taarifa za mwombaji katika mfumo wa usajili ulinasababisha foleni na usumbufu kwa waombaji kutokana na kukaa muda mrefu, kadhalika mamlaka inatumia gharama kuchapa fomu zinazotumika, kufanya manunuzi ya vifaa kwa ajili ya kupakia viambatanisho vya waombaji.

Pia anasema mamlaka inatumia gharama ya kusimamia mchakato wa usajili pamoja na uchakataji wa taarifa za waombaji. Hivyo, Tengeneza anasema mamlaka imejenga mfumo mpya wa usajili ili kumwezesha mwombaji kujisajili kwa njia ya mtandao na kukabiliana na changamoto hizo.

**KUJISAJILI**

Anaongeza kuwa usajili kielektroniki unalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma ya usajili wa raia pamoja na wageni na kwamba ili kujisajiliwa mtandaoni, mwombaji akishaingia katika mtandao wa internet ataandika eonline. nida.go.tz kisha atagonga mahali palipo andikwa jisajili na baada ya hapo, atajaza fomu kwa kufuata maelekezo na kwamba mfumo unamwezesha mwombaji kujaza fomu akiwa popote.

"Baada ya kujaza fomu hiyo, mwombaji anatakiwa kuchapa fomu na kuipeleka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wake kwa ajili ya kugongewa mhuri na saini,"anafafanua na kusema mwombaji anatakiwa kufika katika Ofisi ya NIDA iliyoko katika wilaya yake akiwa na fomu iliyokamilika iliyogongwa mhuri na kuwekwa saini ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, pamoja na nakala za viambatisho vyake alivyopakia katika mfumo wakati wa usajili ili kukamilisha taratibu za usajili (kuhojiwa na uhamiaji na kuchukuliwa alama za vidole ( biometria).

Anasema mfumo mpya wa usajili unampunguzia mtu changamoto mbalimbali zinazotokana na njia inayotumika sasa katika usajili wa taarifa za mwombaji wa vitambulisho vya taifa, anataja faida zipatikanazo serikalini, NIDA pamoja na waombaji kupitia mfumo huo kuwa utatanua wigo wa usajili kwa kusogeza karibu huduma ya usajili kwa raia na wageni wakaazi kwa kuwa utapatikana kila mahali kwa kutumia kifaa chenye uwezo wa kupokea mtandao wa mawasiliano.

"Ujenzi wa mfumo mpya utapunguza gharama zinazotumika katika kuchapisha fomu za usajili na pia kupunguza gharama za uchakataji wa taarifa. Kupunguza usumbufu kwa waombaji wa vitambulisho vya taifa ambao wanafika ofisi za NIDA kwa ajili ya kuchukua fomu ya usajili na kujaza kwa ajili ya maombi ya kitambulisho cha Taifa; kwa kuwa zoezi la ujazaji wa fomu na kuambatanisha viambatisho litafanyika akiwa mahali popote," anataja.

Faida nyingine anaitaja kuwa ni utapunguza muda unaotumika katika kusajili taarifa za mwombaji kwa

kuwa zoezi la kusajili taarifa zao litakuwa limefanywa na mwombaji mwenyewe. Anasema matarajio ya NIDA ni kwamba ujenzi wa mfumo huo mpya utaongeza idadi ya watu wanaohitaji huduma ya usajili kwa kuwa itapatikana mahali popote.

## WANENAVYO MALENGA

### MAISHA NI KANZIDATA

1. MAISHA ni kanzidata, upende na usipende,
Huku wanataka data, upende na usipende,
Kule wanataka data, uende na usiende,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

2. Mikopo ni kanzidata, upende na usipende,
Kama unao utata, hukopi baki ukonde,
Hadi usafishe data, ndipo kukopa uende,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

3. Vidole ni kanzidata, kama wataka kipande,
Hata macho kanzidata, pasipoti uipende,
Kama unao utata, uangushwe kama mende,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

4. Hata picha kanzidata, kokote kule uende,
Kitambulisho utata, hilo kosa usitende,
Kwani watacheki data, na kukusweka rumande,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

5. Mifugo ni kanzidata, ili idadi iende,
Ng'ombe kuku kanzidata, nchi yetu uipende,
Kila kitu kanzidata, kokote kule uende,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

6. Wakubwa ni kanzidata, acha simu wazipende,
Watumiao tafuta, mafanikio tupende,
Wasotumia ni data, watumie sote twende,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

7. Na watoto kanzidata, wakizaliwa tutende,
Chanjo kama wanapata, afya zao tuzipende,
Walo shule taka data, wasome na wasipinde
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

8. Kilimo ni kanzidata, mazao gani tupande,
Mbolea wanaopata, wapi ruzuku iende,
Kotekote leta data, ili uchumi upande,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

9. Barabara kanzidata, maendeleo yaende,
Za lami ni kanzidata, kokoto ngazi zipande,
Tanroad kanzidata, na Tarura ajipinde,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

10. Magonjwa ni kanzidata, chochote kile tutende,
Malaria kanzidata, saratani na matende,
UVIKO ni kanzidata, ripoti kote ziende,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

11. Mipango ni kanzidata, ili hatua tuende,
Kama tukikosa data, ni sawa kifo cha mende,
Tutaokotaokota, hadi migongo ipinde,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

12. Kila kitu kanzidata, huo ndio mwendo twende,
Utakacho utapata, inabidi uzipende,
Acha okotaokota, kutafuta usikonde,
Maisha ni kanzidata, chukueni zote data.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Vyuo vya ufundi 28 kutoa mafunzo uanagenzi kwa wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imesaini makubaliano na vyuo vya ufundi 28 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uanagenzi awamu ya pili kwa vijana 3,765 wakiwamo wenye ulemavu.

Mkurugenzi wa Idara ya Ajira na Ukuzaji Ujuzi wa Ofisi hiyo, Ally Msaki, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha kusaini makubaliano ya kutoa mafunzo hayo jijini hapa.

Msaki alisema mafunzo hayo yanatarajia kuanza karibuni huku akiwataka wawakilishi wa vyuo hivyo kusimamia kwa ufasaha kulingana na elimu ya usimamizi walioupata kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

"Mafunzo haya ni ya awamu ya pili katika mwaka wa fedha 2022/23 ambao tulipanga kuwawezesha vijana 11,525 na kwenye awamu ya kwanza tayari vijana 7,760 wamenufaika na mafunzo hayo," alisema Msaki.

Alisema mafunzo hayo ni ya miezi sita na fani zinazotolewa ni ufundi, umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, useremala, ufundi magari, umeme wa magari, uchomeleaji na uungaji vyuma.

Fani nyingine ni pamoja na utengenezaji wa vifaa vya aluminium, upishi, uhudumu wa hoteli na vinywaji, ushonaji, uchenjuaji wa madini, ufundi bomba, ufundi mwashi, uwekaji wa tarazo na marumaru, ufundi viyoyozi na majokofu.

# Madiwani wataka elimu kudhibiti maambukizi VVU

**Na Elisante John,** SINGIDA

BARAZA la Madiwani la Manispaa ya Singida, limeitaka kamati shirikishi ya kudhibiti Ukimwi kutoa elimu ipasavyo ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) hasa kwa wanawake na wasichana.

Maamuzi hayo yalifikiwa kutokana na taarifa ya Januari hadi Machi, 2023 kuonyesha wanawake 118 na wanamume 50 walipata maambukizi mapya ya VVU, kati ya watu 10,098 waliopima kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya, katika manispaa hiyo.

Wakizungumza kwenye kikao cha baraza hilo robo ya tatu, Diwani Ibrahimu Murua, alisema ni vyema kamati kutoa elimu ya kutosha na kufuatilia kwa karibu baadhi ya maeneo yanayotajwa kuwa wanawake wanajiuza.

"Kuna haja ya Kamati ya kudhibiti Ukimwi kuchukua hatua zaidi, ikiwamo kuongeza kasi ya utoaji elimu ili kuinusuru jamii, hasa wanawake na wasichana wanaolazimika kujiuza kwenye majengo yaliyogeuzwa sasa kuwa madanguro," alisema Murua.

Naye Diwani Mbua Gwae, alisema pia kuna haja kwa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari wapatiwe elimu ya kutosha ili waelewe madhara na ukubwa wa tatizo hilo.

Akiwasilisha taarifa hiyo ya masuala ya Ukimwi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, ambaye ni Naibu Meya Manispaa ya Singida, Hassan Mkata, alisema katika kipindi hicho, hali ya maambukizi ni asilimia 1.7 na kuomba wadau ili kukabili tatizo hilo.

**Naye Diwani Mbua Gwae, alisema pia kuna haja kwa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari wapatiwe elimu ya kutosha ili waelewe madhara na ukubwa wa tatizo hilo.**

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Upendo Naftali, alisema uwapo wa Shirika la AMREF Health Africa (SHIDEPHA) na Faraja Center imeisaidia idara yake kukabiliana na Ukimwi kwenye manispaa hiyo.

"Pamoja na uhamasishaji wa upimaji VVU kwa hiari kwa kushirikiana na mashirika haya, usimamizi wa miradi ya wasichana balehe na wanawake vijana tulipokea fedha Sh. milioni 173, kwa kata zote kupitia mradi wa Timiza Malengo," alisema.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akizungumza na Mbunge wa Ismani CCM, William Lukuvi (wa tatu kulia) na baadhi ya wabunge nje ya ukumbi wa Bunge baada ya kuhudhuria majadiliano ya kikao cha Bunge mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya 300,000 wachunguzwa macho kuepushwa upofu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Sightsavers limewafanyia uchunguzi wa macho watu 343,263 wa Mkoa wa Singida ili kuwaepusha na upofu.

Mratibu wa Mradi wa Mtoto Angaza wa shirika hilo, Upendo Minja, aliyasema mwishoni mwa wiki mjini hapa wakati wa kikao cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi huo.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Februari 2021 tangu mradi huo ulipoanza hadi Machi 2023 watoto 343,263 wamefikiwa kwa kuchunguzwa kama wana matatizo ya macho kati ya lengo lililokuwa limewekwa na mradi la kuwafikia watoto 308,696.

Naye Katibu Tawala mkoani humo, Dk. Fatma Mganga, akifunga kikao hicho, aliwataka wataalamu wa afya kutoa elimu kwenye shule na jamii kwa ujumla kuhusu ulaji wa lishe bora itakayosaidia kuondoa tatizo la uoni hafifu.

Aliwataka Maofisa Lishe na Maofisa Kilimo mkoani humo kutoa elimu na kusaidia wananchi kwenye kilimo cha bustani ili kulima mazao yenye virutubisho vitakavyosaidia kuongeza ulinzi wa macho.

Dk. Mganga aliagiza kusambaza mkoa mzima taarifa za uwapo wa huduma ya matibabu kwa gharama nafuu yanayoendelea katika Hospitali ya Rufani Mandewa zifikishwe kwa jamii husika kwa kuwa wengi wana tatizo, lakini hawajui wapi pa kupata msaada.

Alisema uoni hafifu unachangia kushuka kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na kushuka viwango vya elimu.

"Endapo walimu hawataweza kuwapanga watoto darasani kulingana na uwezo wa macho yao watoe maelekezo kwa walimu kuhakikisha kunakuwa na mpangilio wa ukaaji darasani," alisema.

Meneja miradi ya Sightsavers, Edwini Maleko, alisema Mkoa wa Singida umefaidika na miradi inayotolewa na shirika hilo kwa kuwa zaidi ya Shilingi bilioni saba zimetumika.

"Fedha hizi zimetumika kwenye ujenzi wa nyumba, vifaa tiba na kusomesha watumishi wa afya katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na nchini India," alisema.

Maleko alisema tatizo la uoni hafifu mkoani Singida ni kubwa na asilimia 2.8 wana ulemavu wa macho na wanatakiwa kupata matibabu ili kuondokana na kadhia hiyo.





# W'biashara wanne mbaroni kutumia stakabadhi chini kiwango walichouza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wanne wamekamatwa na Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kwa kosa la kuchukua stakabadhi za bidhaa walizonunua zikiwa zimeandikwa kiwango kidogo cha fedha kuliko gharama halisi ya bidhaa walizonunua.

Kukamatwa kwa wafanyabiashara hao kunatokana na hatua ya maofisa wa TRA kuingia mitaani kuendesha kampeni iliyopewa jina la 'Tuwajibike' yenye lengo la kutoa elimu na kuhamasisha wananchi na wafanyabiashara kudai na kutoa stakabadhi kila wanapofanya ununuzi.

Akizungumza baada ya kuwakamata wafanyabiashara hao, Ofisa wa TRA mkoani Mbeya, Albert Chamba, alisema katika operesheni hiyo ya Tuwajibike wanaanza kwa kutoa elimu kwa wananchi na kisha kufanya operesheni ya kuwakamata wale ambao hawatokabadhi na wasiodai stakabadhi wakati wa kufanya ununuzi.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo wamebaini changamoto kubwa mbili ambazo zinaifanya serikali kutopata mapato inayostahili kutokana na watu kutodai au kutoa risiti wakati wa kufanya biashara.

"Katika kampeni yetu ya tuwajibike tumebaini kuwa kuna wafanyabiashara ambao wanatoa stakabadhi vizuri, lakini wanafanya udanganyifu kwa kuandika kiwango kidogo kwenye stakabadhi kuliko kiwango cha fedha walichopokea, lakini changamoto ya pili ni baadhi yao kutotoa kabisa stakabadhi," alisema Chamba.

Alisema mambo yote mawili ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na kwamba kutokana na kosa hilo wamewakamata wafanyabiashara wanne.

Alisema miongoni mwa wafanyabiashara hao wanne, kati yao watatu walikuwa na stakabadhi ambazo zimeandikwa viwango vidogo vya fedha kuliko kiasi cha fedha kilichotolewa na mmoja hakuwa na stakabadhi kabisa.

Baadhi ya wafanyabiashara waliokamatwa wakiwa na stakabadhi zilizoandiwa viwango vidogo kuliko fedha halisi walizolipa, walisema kuwa wanafanya hivyo ili kupata unafuu kidogo wa kodi wanazopaswa kulipa serikalini. "Tunapokwenda kununua bidhaa kwenye maduka ya jumla wakati mwingine huwa tunaomba kupunguziwa kidogo bei, tunapokuwa tumepunguziwa, wenzetu nao hutuomba kupunguza kiwango cha fedha wanachotuandikia kwenye stakabadhi wakidai kuwa wakiandika uhalisia watatakiwa kulipa kodi kubwa serikalini, hiyo ndiyo sababu tunapokea stakabadhi zenye viwango pungufu," alisema Ibrahim Khalfan ambaye ni mfanyabiashara wa kijiji cha Igurusi aliyefika jijini Mbeya kununua bidhaa za dukani kwake.

Joyce Mwakipesile, ambaye alikamatwa akiwa na bidhaa bila stakabadhi, alisema alidai stakabadhi na akapewa lakini kwa bahati mbaya aliipoteza wakati wakisafirisha bidhaa zake kutoka dukani kwenda kwenye kituo cha basi.

Alisema upo umuhimu wa mifumo ya kodi kuweka kumbukumbu ili inapotokea mteja akapoteza stakabadhi yake aweze kurudi dukani na kuchukua nakala ili kuondoa sintofahamu kama iliyomkuta.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Musibu Shaban, alisema kitendo cha kutotoa au kutodai stakabadhi wakati wa kufanya manunuzi ni kosa kisheria ambalo linaweza kusababisha mhusika kupata adhabu ya faini au kifungo.

Alisema kwa mfanyabiashara asiyetoa au kufanya udanganyifu kwenye stakabadhi anaweza kutozwa faini ya kati ya Sh. milioni 1.5 hadi Shilingi milioni tatu.

"Kwa upande wa mteja aliyenunua bidhaa bila kudai au kupokea risiti ambayo imeandikwa kiwango kidogo cha fedha kuliko uhalisia wa fedha aliyolipa, anaweza kutozwa faini ya kati Sh. 30,000 na Sh. milioni 1.5," alisema Shaban.



Maofisa Elimu wa Wilaya na Kata wa Mkoa wa Mbeya wakishiriki kikao cha tathmini ya elimu kilichoitishwa na Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Ernest Hinju, kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Hospitali yatoa mafunzo magonjwa ya damu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, imeanza kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya wa hospitali za wilaya kuhusu magonjwa ya damu ukiwamo ugonjwa wa kuganda kwa damu ujulikanao kwa jina la Hemofilia ili kuongeza uwezo wa kuyakabili.

Juzi madaktari bingwa wa magonjwa hayo walitoa mafunzo kwa watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya ambako kunadaiwa kuwa na ongezeko la watu wanaosumbuliwa na magonjwa ya damu.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya Damu wa Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya, Dk. Mathia Ishengoma, alisema waliamua kuanza kutoa mafunzo hayo ili wagonjwa hao wanapopatikana wawe wanapata huduma mapema.

Alisema baadhi ya wagonjwa wamekuwa wakibainika kuwa na magonjwa hayo na kulazimika kupelekwa katika hospitali ya kanda jambo linaloweza kuhatarisha zaidi maisha yao.

"Tunaamini kwamba kwa kutoa mafunzo haya wagonjwa watakaokuwa wanapatikana watapata huduma kwa haraka zaidi ili kupunguza madhara ya magonjwa haya ya damu," alisema Dk. Ishengoma.

Alisema mafunzo hayo yaliwahusisha watumishi wote wa hospitali ili kupanua zaidi wigo wa utoaji huduma hizo kwa wananchi wa maeneo hayo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo waliwashukuru madaktari bingwa hao kwa kuwapatia mafunzo hayo wakieleza kuwa ni miongoni mwa nyenzo muhimu ambazo watazitumia katika kuokoa maisha ya wananchi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Dk. Ally Msonga, alisema mafunzo hayo yaliwapatia utaalamu wa kuwahudumia wananchi watakaobainika kuwa na matatizo hayo kwa weledi tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema magonjwa ya damu huwa hayawakumbi mara kwa mara wananchi, lakini wanahitaji kujiandaa ili inapotokea wawe na uwezo wa kuyakabili kirahisi.

"Tunashukuru wametuongezea nyenzo muhimu sana, tutaendelea na sisi kuusambaza huu ujuzi kwenye maeneo ya vijijini ili kupanua zaidi huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye hivi vituo vikubwa," alisema Dk. Msongo.

Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Pascalina Mwaipopo, alisema mafunzo waliyoyapata yatawasaidia kuwatambua watu wenye matatizo ya hemofilia na kuwatibu kirahisi.

Alisema pia watakuwa na uwezo wa kuwahudumia vizuri bila kutegemea kuwapeleka Mbeya kwenda kutibwa na kwamba watahakikisha wanasambaza utaalamu huo mpaka kwenye vituo vidogo vya kutolea huduma.

# Mikoa 14 Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaathirika tindikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya asilimia 14 ya ardhi inayofaa kwa kilimo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imeathirika kwa kuwa na kiwango kikubwa cha tindikali hali inayosababisha wakulima kukosa tija ya uzalishaji wa mazao.

Mtafiti wa Afya ya Udongo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) kituo cha uyole jijini hapo, Fredric Mlowe, aliyasema hayo wakati wa mkutano wa wadau mbalimbali wa kilimo uliokuwa na lengo la kuwasilisha taarifa ya ugunduzi wa chokaa ya kudhibiti tindikali.

Wadau walioshiriki kwenye kikao hicho ni wataalamu wa utafiti kutoka TARI, wataalamu kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na maofisa kutoka katika Kiwanda cha Saruji cha Mbeya ambacho ndicho kitazalisha chokaa hiyo.

Alisema hali hiyo inasababisha uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula kushuka kutokana na mazao hayo kushindwa kufyonza virutubisho vinavyowekwa kwa ajili ya kunenepesha mazao hayo.

"Utafiti unaonyesha kwamba ekari moja ya mahindi mtu anatakiwa kuvuna tani tatu na zaidi, lakini kiwango hicho katika mikoa yetu hakifikiwi kwa sababu mazao hayo yanashindwa kufyonza vizuri mbolea inayowekwa na hivyo nyingi inapotea," alisema Mlowe.

Alisema njia pekee ya kupunguza tindikali hiyo ni kutumia chokaa ambayo kitaalamu inafanya kazi ya kufyonza tindikali kutokana na kuwa na madini ya calcium ambayo yanashusha tindikali hiyo chini na hivyo kuchuja udongo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Juliana Mwakasendo, alisema baada ya kubaini hali hiyo kwenye udongo, wameanza kuhamasisha wananchi kutumia chokaa kupunguza tindikali hizo.

Alisema teknolojia hiyo ya kutumia chokaa ni muhimu na ikitumika ipasavyo itasaidia kupunguza tindikali hizo na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula.

"Baada ya kukamilisha utoaji wa elimu tutaanza kusambaza chokaa hii kwa wakulima, tunaamini kwamba wakulima wetu wakihamasika kuitumia na wakafuata utaalamu wote hata uzalishaji wa mazao utaongezeka," alisema Dk. Juliana.

Alisema jukumu la kuzalisha chokaa hiyo na kuwafikishia wakulima, wamelikabidhi kwa kiwanda cha saruji cha Mbeya na wamekubaliana viwango vinavyotakiwa na kwamba wataendelea kufuatilia.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya, Khaled Ghareob, alisema watahakikisha wanazalisha chokaa ya kutosha na kuisambaza kwa wakulima ili waendelee kuitumia kwenye mashamba yao na hivyo kukidhi malengo ya kupunguza tindikali.

Alisema mbali na kufanya biashara pia wanafanyakazi ya kuisaidia jamii kwa kuhakikisha wanawasaidia wakulima ambao ni sehemu ya jamii hasa kuwasaidia kwenye uzalishaji.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwenye hafla hiyo, Jaffari Haniu, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, aliwasisitiza wakulima kutumia teknolojia hiyo ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao.

Alisema matumizi ya chokaa hiyo ni sawa na kukarabati nyumba na hivyo akawataka wananchi kufanya hivyo ili kuongeza virutubisho kwenye udongo.



## Mradi kupima udongo kuwezesha wakulima kilimo bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema tayari inatekeleza mradi wa kupima udongo ambao utawawezesha wakulima kufahamu aina gani ya mazao yanayohitajika kulimwa katika eneo husika kutokana na matokeo ya utafiti wa udongo husika.

Hayo yalisemwa jana na waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, wakati akijibu swali la mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib aliyetaka kujua utafiti wa udongo kwa ajili ya kuotesha mazao husika kwa wakulima lini utafanyika.

Alisema mradi huo tayari umezinduliwa na lengo lake kubwa utawawezesha wakulima kulima kwa uhakika baada ya udongo husika kufanyiwa utafiti na wataalamu.

Shamata alisema utafiti wa kazi za kupima udongo utafanywa na kituo cha utafiti kilichopo Kizimbani Unguja kupitia maabara yake katika mradi ambao tayari umezinduliwa hivi karibuni.

"Tayari wizara tumezindua maabara ya kupima udongo ambao matokeo yake yatawawezesha wakulima kulima mazao na kupata matokeo mazuri ya mavuno," alisema.

Aliwataka wakulima wanaoendesha kilimo cha maweni kulima mazao yanayostahimili ukame ikiwamo mtama, kunde pamoja na muhogo.

Alisema mazao hayo ni ya asili kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya Maweni ambayo yanastawi vizuri na kuongeza kipato cha wakulima.

# 'Marufuku kusoma nje kozi zinazopatikana ndani ya nchi'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdul Gulamu, amesema uongozi wa wizara hiyo umepiga marufuku kupeleka wanafunzi nje ya nchi kwa njia ya mikopo kwa kozi zinazosomeshwa na kupatikana kwa vyuo vya ndani ya nchi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Professa Omar Fakihi Hamad, aliyetaka kujua ni wanafunzi wangapi waliopelekwa kusoma nchini Uganda ambao wanaendelea na masomo na hawajalipwa fedha za kujikimu.

Naibu Waziri alisema, katika kusomesha wanafunzi nje ya nchi kwa kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, umewekwa utaratibu unaowataka wanafunzi kuchangia gharama za masomo.

Alisema hali hiyo inatokana na ukubwa wa gharama za masomo kwa vyuo vya nje, lakini kushajihisha wanafunzi wa ndani kutumia vyuo vikuu vya ndani kwa kozi zinazopatikana ndani ya nchi ambazo gharama zake ni nafuu.

"Utaratibu uliopo, mwanafunzi husika aliyekubaliwa kusoma nje ya nchi hutakiwa kuchagua moja kati ya njia mbili ambazo ni apatiwe mkopo wa kulipiwa ada pekee kwa asilimia100 au apatiwe mkopo kwa kulipiwa posho ya kujikimu kwa ajili ya malazi na chakula pekee," alisema Gulamu.

Aidha, alisema kwa mwaka 2022/2023 jumla ya wanafunzi wanaolendelea na masomo nchini Uganda kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni 65 wakiwa wanasoma katika vyuo tisa.

Alisema kati ya wanafunzi 65 waliopo Uganda ni mmoja pekee anayesoma Chuo Kikuu cha Makerere aliyechagua utaratibu wa kulipwa posho.

"Wanafunzi 64 waliosalia wote wanatumia utaratibu wa kulipiwa ada katika vyuo vyao. Hakuna posho za nyuma zinazodaiwa na wanafunzi hao wa Uganda kwa vile makubaliano ni kuwalipia ada ya masomo na mitihani tu na maamuzi hayo yanatekelezwa kikamilifu," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, akimkabidhi Spika wa Baraza la Wawakilishi ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ofisini kwake Chukwani Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yajipanga kukabiliana mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amesema mabadiliko ya tabianchi ni moja kati ya changamoto za kidunia na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira ya baharini katika maeneo ambayo yapo chini ya usimamizi wa hifadhi za bahari kwa ajili ya kulinda rasilimali zake.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, Said Saleh, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo.

Alisema maeneo mbalimbali ya visiwa vya Zanzibar yameathiriwa na mabadiliko hayo ikiwamo eneo la Tumbe bandarini.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, imefanya juhudi za kuyanusuru maeneo hayo ikiwamo la Tumbe Bandarini.

Alitaja miongoni mwa juhudi hizo ni upandaji wa miti na kupitia mradi wa LDCF, jumla ya miti 2,000 ya aina ya mikungu na mivinje ilipandwa kwa kushirikana na Jumuiya za Vijana Tumbe (JMVT).

"Serikali kupitia ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Idara ya Mazingira, tulipanda miti aina ya mikoko ekari kumi katika eneo la Mwanasoza hadi Pondeani, eneo ambalo limeungana na bandari kwa lengo la kusaidia kuyadhibiti maji ya bahari yasiingie kwa nguvu katika eneo la bandari," alisema.

Aidha, alisema ofisi yake inatoa elimu kwa wanajamii kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na namna ya kupambana nazo.

"Pamoja na kushajihisha jamii katika kupanda miti ya juu na ya pwani (mikandaa) ili kupuguza athari hizo. Kupitia suala hili la Mhe. Mwakilishi, natoa wito kwa wananchi kuwa na tabia ya kupenda kuotesha miti," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SABRINA HAMISI SIMBA** anatangaza kupotelewa na Equivalence Certificate chenye namba U1665/024 kilichotolewa na **HANA INTERNATIONAL SCHOOL UGANDA** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBD/RB/1840/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na.638/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU PILI SHABAN KONDO WA TEMEKE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA HEMED NASIB ABDALLAH**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 28 Mwezi 04 Mwaka 2023

HAKIMU

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA
DAR ES SAL

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 104 YA MWAKA 2023**

**SHARIFA S. MGAZA ..............................................MDAI**

**VERSUS**

**OMARY MHINA ..............................................MDAIWA**

**KWA:**
**OMARY MHINA**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 17.05. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 15 ya mwezi wa MEI, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**NDASKOY ITAELY MUNISI,** Anatangaza kupotea kwa kadi mbili za pikipiki, ya kwanza yenye namba za usajili MC 185 BFK aina ya GSM, Chassis No. **LV7MKA404FA905580,** Engine No. **162FMJ1506063042.** Ya pili aina ya **BAJAJ BOXER** yenye namba za usajili **MC 131 CMW.** kwa yeyote atakaezione atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/165543/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LIKIJIYE MELITA MOLLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TRACTOR** yenye usajili namba: **T 374 AZJ, CHASSIS** NAMBA: **6T3X154830** na ENGINE NAMBA: **152EA29376D.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/165709/2023**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ENOCK ERNEST LYIMO** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 092700** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **01 March, 2019.** Mwisho wa Matumizi ni tarehe 28 Feb 2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/152351/2023.**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT**
**AT TUKUYU**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 02/2023**

**In the Matter of the Estate of the Late AFYUSISYE TUNKONGE**

**And**

**REHEMA AFYUSISYE KAMESA................1ST APPLICANT**
**ALINIKISA AFYUSISYE KAMESA............2ND APPLICANT**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grand of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 30th day of June, 2023.

Dated at Rungwe this **10th day of May, 2023.**

R.I. SHEHAGILO
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**STANFORD GODSON MMASSA** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye index namba: **PS1102089-021** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya msingi MAMBOYA mwaka 2015 na cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S4745/0016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari MAMBOYA. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **MOR/MOR/RB/450524/2022**

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**AFFIDAVIT**
**(Made in Declaration and Verification and Usage of Names)**

**I, HILDA NAHUM MARO,** a Tanzania Citizen and a Christian and now leaving at Mbezi-Luis, Ubungo District, Dar es salaam Region, do hereby solemnly SWEAR and declare that:-

1) Iam the solemn declarant herein and verily conversant with the facts deponed to herein.
2) That Ia m a Tanzania and now leaving at Mbezi Luis, within Ubungo District, Dar es salaam Region and that I have used the name of **HILDA NAHUM MARO** on my National Identification card with reference No: 19600708-11467-00001-14 and the same name has been used in my other personal records and transactions.
3) That upon contracting my lawfull marriage, I used the name of HILDA NAHUM LATELA and it is the same name that I have used in filling up my application for retirement benefits.
4) Further, I have used the name of HILDA NAHUM LATELA on my Driving License with reference No: 4000000798 dated 30th September, 2019.
5) That I further declare that the name of **HILDA NAHUM MARO** and **HILDA NAHUM LATELA** all refer to one and the same person.
6) That I make the solemn declaration consciously believing the same to be true by virtue of the Oath's and Statutory Declaration Act, RE. 2002.

Sworn at Dar es Salaam by the said HILDA NAHUM MARO who is Known to me personally this 7th Day of September, 2020

DEPONENT



Before Me
Name:
Address:
Qualification:
Signature:

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Morogoro**
**Kituo cha Mjini Mkoa Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi Na. 42/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU RASHIDI KISWANYA WA KONGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA**
**RASHIDI IDD KIMANGA**
**TANGAZO**
*Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za Usimamizi w a Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu , wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **1 mwezi 05 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye Wosia na Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa .

Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika

**Imetolewa tarehe 9 mwezi 05 mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

---

Uza, Chenye Thamani

Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Uchaguzi mkuu Uturuki ngoma mbichi

**ANKARA,** Uturuki

USHINDANI mkali bado umeendelea kuonekana katika uchaguzi mkuu wa nchini Uturuki baada ya Rais Recep Erdogan kuona uwezekano wa kufanyika uchaguzi kwa awamu ya pili kwa sababu awamu ya kwanza hakuna upande uliopata zaidi ya asimilia 50 ya kura.

Kwa mujibu wa taarifa ya shirika la habari la serikali ya Uturuki Anadolu, mfungamano wa vyama unaoongozwa na Rais Erdogan ulipata asilimia 49.39 ya kura wakati mfungamano wa vyama sita vya upinzani unaoongozwa na Kemal Kilicdaroglu ulifikia asislimia 44.92.

**Hadi sasa zaidi ya asilimia 90 ya kura zote zilizopigwa zimeshahesabiwa na kwamba duru ya pili ya uchaguzi huenda ikafanyika Mei 28, mwaka huu.**

Ilielezwa kuwa hadi sasa zaidi ya asilimia 90 ya kura zote zilizopigwa zimeshahesabiwa na kwamba duru ya pili ya uchaguzi huenda ikafanyika Mei 28, mwaka huu.

Taarifa zinaeleza kuwa matokeo, kamili yatajulikana baada ya duru ya pili ya upigaji kura iwapo itaamriwa hivyo na tume ya uchaguzi na kwamba ndio yataamua kama nchi ya Uturuki, itatawaliwa na Erdogan au utawala utachukuliwa na mpinzani wake mkuu Kemal Kilicdaroglu.

Akizungumza na wafuasi wake mjini Ankara, Erdogan, aliwaambia kwamba ana imani kubwa ya kuibuka mshindi lakini ataheshimu uamuzi wa tume ya taifa ya uchaguzi iwapo itaamuru kinyang'anyiro hicho kirudiwe katika duru ya pili, ambayo endapo itabidi ifanyike basi uchaguzi utafanyika kwa wiki mbili.

Naye Kilicdaroglu, alisema ana kila sababu ya kuamini kuwa yeye ndiye atakayeshinda iwapo wananchi wa Uturuki watalazimika kupiga kura ya marudio.

Uchaguzi wa mwaka huu wa nchini Uturuki kwa kiasi kikubwa ulijikita katika masuala ya ndani kama vile uchumi, haki za kiraia na mkasa wa tetemeko la ardhi la mwezi Februari ambako zaidi ya watu 50,000 walipoteza maisha.

Wakati huo huo macho yote yanamwangalia sasa mgombea binafsi Sinan Ogan, aliyepata asilimia tano ya kura, huku akisubiriwa kuwa atakwenda upande gani.

Inaelezwa kuwa Ogan alifukuzwa kutoka kwenye chama cha watu wasiopendelea siasa kali ambacho miezi michache kabla ya uchaguzi kiliungana na Erdogan na kumfanyia kampeni.

Hata hivyo alisema atatoa uamuzi baada ya kufanya mashauriano na wawakilishi wa vyama vyote. **DW**

## Jenerali Burhan afungia akaunti za mpinzani wake

**KHARTOUM,** Sudan

MKUU wa Jeshi la Sudan, Jenerali Abdel al-Burhan, ametoa agizo la kufungia akaunti za benki za kundi la wanamgambo wa Rapid Support Forces (RSF) na kampuni zake tanzu.

Taarifa zilieleza kuwa Jenerali Burhan alitoa amri hiyo jana, sambamba na kustaafisha maofisa wanne wa kijeshi wanaohusishwa na kundi hilo la RSF.

Mmoja wa maofisa walioathiriwa ni Bregedia Jenerali Omar Ahmed, kamanda wa RSF Jenerali Mohammed Dagalo, ambaye kwa sasa anaongoza ujumbe wa jeshi la wanamgambo kwa mazungumzo ya amani na jeshi la Sudan huko Jeddah, Saudi Arabia.

Jenerali Burhan pia alimfuta kazi gavana wa benki kuu Hussain Jankol na kumteua Borai El Siddia ili kuziba nafasi yake, na kwamba hakutoa sababu ya kumfuta kazi aliyekuwa kiongozi wa benki nchini humo Jankol.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa chaneli ya serikali ya Sudan TV, ilianza tena kurusha matangazo yake ya satelaiti mwishoni mwa wiki iliyopita, ikiwa ni wiki moja baada ya kutokwenda hewani.

Pia ilielezwa kuwa usambazaji wa kituo hicho uliathirika mara kadhaa tangu mapigano kati ya jeshi na RSF kuanza Aprili 15, mwaka huu. **BBC**





Nyumba zikionekana kudondoka na zingine kuharibiwa vibaya ikiwa ni moja ya madhara yaliyotokana na mafuriko yaliyoikumba DRC wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

## Waathiriwa wa mafuriko washutumu utaratibu ugawaji misaada DRC

**KINSHASA,** DRC

WAATHIRIWA wa mafuriko yaliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 400 Kivu kusini, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wameonyesha kusikitishwa baada ya kuona usambazaji wa misaada ya kibinadamu unafanyika kwa njia ya machafuko.

Baadhi ya waathiriwa wa maporomoko ya udongo wa wilayani Kalehe, walisema wamejutia kile wanachokisema ubaguzi usioelezeka ulioonekana wakati wa usamabazaji wa misaada iliyopelekwa huko na mashirika ya misaada juzi.

Inaelezwa kuwa sehemu kubwa ya msaada huo ulielekezwa zaidi kwa wakazi wa kijiji cha Bushushu, wakati wakazi wa vijiji kadhaa Nyamukubi na Bushushu ndio walipaswa kupewa misaada hiyo kwa usawa.

Misaada hiyo ni pamoja na mavazi, mahema na mabati, huku mashuhuda wakisema kulitokea vurugu wakati wa ugavi.

Tukio hili ni la pili kutokea baada ya majanga mengine asilia kushuhudiwa mwaka 2014, kama anavyoeleza Désiré Makuta.

"Hapo awali hatukujua kuwa pale tulipo majanga yangeweza kutokea ilikuwa ni mara ya kwanza lakini nakumbuka Septemba 12, 2012, kulikuwa na watu tisa ambao walipoteza maisha pale na ili kufika mahali ilipotokea janga hilo asilia, ni umbali wa kilomita moja tu," alisema Makuta. **RFI**

## Tuhuma njama za mapinduzi zawasweka ndani 11

**N'DJAMENA,** Chad

MWANASHERIA Mkuu wa nchini Chad ameliambia shirika la habari la (AFP) kuwa watu 11 wanaoshutumiwa kupanga njama za mapinduzi nchini humo wamehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela, huku Rais wa taifa hilo akisema kuwa watasamehewa.

Mapema Januari mwaka huu, serikali ilitangaza kwamba maofisa 10 wa jeshi na mwanaharati maarufu wa haki za binadamu Berdei Targuio walikamatwa wakishutumiwa kujaribu kuvuruga utaratibu wa kikatiba na taasisi za nchi.

Berdei Targuio aliyetambulishwa na mamlaka kama kiongozi wa mpango huo wa kufanya mapinduzi mwezi Desemba, ni mwenyekiti wa shirika la kutetea haki za binadamu la Chad (OTDH) na mkosoaji mkubwa wa utawala.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Chad, watuhumiwa hao 11, ambao wamezuiliwa katika gereza lenye ulinzi mkali la Koro Toro, lililoko kaskazini mwa mji mkuu, walihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa kuvunja utaratibu wa kikatiba, kumiliki silaha kinyume cha sheria na kushirikiana na wahalifu.

Ilielezwa kuwa licha ya hukumu hiyo na tuhuma zinazowakabili watu hao 11, Rais wa Chad Jenerali Mahamat Deby aliapa kuwaachia huru.

"Rais atatekeleza ahadi yake," msemaji wa ikulu Brah Mahamat aliiambia AFP, akiongeza kwamba lazima hukumu itangazwe kabla ya msamaha wa rais kutolewa. **VOA**

# 'NAMUNGO ILISTAHILI USHINDI KWA AZAM'

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Kalimangonga Ongalla, amesema wapinzani wao, Namungo FC, walistahili kupata ushindi dhidi yao kwa sababu walicheza vizuri na wachezaji wake walijituma zaidi.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, raundi ya 28, kati ya timu hizo na Namungo ikiibuka na ushindi wa 2-1, mechi ikipigwa Uwanja wa Chamazi, Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, Kally alisema hakuna kitu chochote ambacho wachezaji wake wangekifanya ili kuwazuia wapinzani wao ambao walicheza kandanda safi na la kuvutia.

**"Leo [juzi] hakuna kichofanyika wala kukamilika, hatukustahili kushinda, tumecheza chini ya kiwango na wapinzani wetu walikuwa bora sana. Kwa jinsi tulivyocheza Namungo walistahili kushinda na ninawapongeza kwa hilo," alisema Kally.**

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, alisema wamekuwa kwenye kiwango kizuri katika michezo miwili mfululizo dhidi ya Simba na Azam Fc pia, hivyo inaonekana kuwa wachezaji wake wameshika mafunzo yake kwa ukamilifu.

"Baada ya mchezo wa Simba tulipata sare, tulikuwa na kiwango kizuri, vijana walingia kwa ari kwenye mechi hii tuliruhusu bao la kwanza, lakini wachezaji wakapambana wakarudisha, goli la pili lilivyotengenezwa na kufungwa lilikuwa kali sana na limenifurahisha," alisema kocha huyo.

Kabla ya kuvaana kwenye mechi ya juzi, timu hizo zote mbili zilicheza dhidi ya Simba, Namungo ikicheza kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi katika mechi ya raundi ya 27, Mei 3 na kutoka sare ya bao 1-1, Azam nayo ikicheza dhidi ya Simba Mei 7, mwaka huu kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA na kushinda mabao 2-1.

Pamoja na kufungwa, Azam bado imesalia nafasi ya tatu na pointi zake 53, Namungo ikipanda mpaka nafasi ya tano, ikifikisha pointi 39.

KOMBE...




Wachezaji wa Timu ya JKT Tanzania, wakishangilia kwa kutwaa kombe kutokana na kuhitimisha Ligi ya Championship [Daraja la Kwanza Tanzania Bara] wakiwa kileleni baada ya juzi kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Trans Camp, katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: JUNMANNE JUMA**

# Mabadiliko makubwa ya soka Mkoa wa Mjini Magharibi yaja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar, kinatarajia kufanya mabadiliko makubwa katika miaka hii minne ili kufikia lengo la kuwa na ligi bora yenye ushindani mkoani humo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Maalim Ahmada, alisema baada ya kumaliza uchaguzi uliofanyika mapema Aprili mwaka huu, wanadhima kubwa kuhakikisha mkoa huo unakuwa na ligi bora kama walivyoanza.

Alisema hatua ya kwanza watakayoanza nayo ni kuwa na mpango mkakati wa miaka minne ambao utaonesha mustakabali mzima wa kufikia maendeleo ya kisoka kuanzia ngazi ya mkoa na wilaya zake tatu zilizopo ndani ya mkoa huo.

Alisema miongoni mwa mipango hiyo ni kuangalia upya namna ya uendeshaji wa Ligi za Vijana ngazi za Wilaya zilizopo katika Wilaya za Mkoa huo ili kuhakikisha zinakuwa na lengo lililokusudiwa la uanzishwaji wake.

Alisema nguzo kubwa ya maendeleo ya soka duniani huanzia ngazi za chini, hivyo wameona ipo haja kuhakikisha soka katika ngazi za wilaya mpaka mkoa kuna kuwa na muundo mzuri.

"Miongoni mwa jambo kubwa tulilolíona kwanza ni kuhakikisha tunakuwa na muundo mzuri wa Ligi za Vijana zile zilizopo wilayani kwa Mkoa wa Mjini Magharibi tuna Wilaya tatu ambazo ni Wilaya Majini, Magharibi A na Magharib B, hivyo lazima tukae na viongozi wa hizi wilaya tuone namna bora ya uwendeshaji wa hizi ligi," alisema.

Aidha, kuhusu kuboresha Ligi ya Mkoa huo, alisema njia ya kwanza ni kutafuta udhamini utakaoleta hamasa kubwa kwa klabu na kuiwezesha kuwa ya ushindani kutokana na udhamini huo.

Alisema tayari Kamati ya Habari na Masoko ya Chama hicho, inaendelea na mchakato wa kuzungumza na kampuni mbalimbali ili kuona msimu mpya wa ligi hiyo wa 2023/24, utakaponza unakuwa na udhamini.

# Yanga U-17 yawa tishio Ligi ya TFF

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya tatu ya Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kwa vijana chini ya umri wa miaka 17, imeendelea tena juzi, huku kikosi cha vijana wa Yanga kikipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Transit Camp, hivyo kucheza jumla ya mechi tatu bila wavu wake kutikiswa.

Hata hivyo, imeshindwa kuweka rekodi ya kushinda mabao 6-0 kama ilivyofanya kwenye mechi mbili zilizopita.

Yanga ilianza ligi hiyo inayopigwa kwenye Uwanja wa Kituo cha Ufundi TFF Kigamboni kwa kuivurumusha African Sports mabao 6-0, kabla ya kushinda kwa idadi hiyo ya mabao kwa mara ya pili dhidi ya Green Warriors.

Ni matokeo yanayofanya kuendelea kusimama juu ya msimamo wa ligi ikiwa na pointi tisa, ikishinda mechi zote tatu.

Mabao ya washindi yaliwekwa wavuni na Mahmoud Bugoma, Nasri Halifa na Ahmed Mohamed.

Wakati vijana wa Yanga wakifanya vitu vyao, kikosi cha Simba chini ya miaka hiyo nacho kikaiadhibu KMC mabao 2-0, moja likiwa ni la kujifungwa mwenyewe, Steven Kimaro, na lingine likiwekwa kwenye kamba na Hamis Salum.

Kwa matokeo hayo, Simba inafikisha jumla ya pointi saba kwani mechi iliyopita iliifunga JKT Tanzania bao 1-0, lakini mchezo wa ufunguzi ililazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Ihefu.

Matokeo mengine ya ligi hiyo, Ruvu Shooting ilitoka sare ya bao 2-2 dhidi ya Singida Big Stars, African Lyon ikaitwanga JKU Academy 3-1, Azam ikaibugiza Pan African 4-0, Mbeya Kwanza na Karume Youth Centre zikatoka sare ya bao 1-1, Ihefu ikaiadhibu JKT Tanzania 2-0 na African Sports ikashinda 1-0 dhidi ya Green Warriors.

**Wakati vijana wa Yanga wakifanya vitu vyao, kikosi cha Simba chini ya miaka hiyo nacho kikaiadhibu KMC mabao 2-0, moja likiwa ni la kujifungwa mwenyewe, Steven Kimaro, na lingine likiwekwa kwenye kamba na Hamis Salum.**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### MBAPPE NA REAL MADRID

KLABU ya Real Madrid bado ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Paris St-Germain. ***(Marca)***

#### RABIOT AWINDWA UNITED

MANCHESTER United inamwinda tena kiungo Adrien Rabiot huku Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 28, akikaribia mwisho wa mkataba wake na Juventus. ***(L'Equipe)***

#### POCHETTINO MIAKA MITATU

MAURUCIO Pochettino anakaribia kusaini mkataba wa miaka mitatu kuwa kocha mkuu wa Chelsea. ***(Telegraph)***

#### CAICEDO KUONDOKA BRIGHTON

KOCHA wa Brighton, Roberto De Zerbi, anatarajia kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo, na kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister (24), kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. ***(Metro)***

#### KOMPANY, WEGHORST KUTETA

MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Wout Weghorst, atafanya mazungumzo na Kocha wa Burnley, Vincent Kompany, baada ya muda wake wa mkopo kumalizika Manchester United. ***(Sun)***

#### RICE KWA UTD, ARSENAL

KLABU ya Manchester United iko tayari kumenyana na Arsenal na Chelsea kwa ajili ya kuinasa saini ya Declan Rice, 24, baada ya kufurahishwa na kiwango cha kiungo huyo wa England akiwa na West Ham dhidi ya 'Mashetani Wekundu', Jumapili. ***(Sun)***

#### AIVUTIA WEST HAM

WEST Ham inavutiwa na mshambuliaji wa Coventry City mwenye umri wa miaka 24, Viktor Gyokeres. ***(Mirror)***

#### SAKA MKATABA MPYA

ARSENAL ina matumaini kuwa winga wa England, Bukayo Saka, mwenye umri wa miaka 21, atasaini mkataba mpya wa miaka mitano ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki kabla ya mwisho wa msimu huu. ***(TalkSPORT)***

#### AUGUSTO NA NEWCASTLE

NEWCASTLE United ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazotarajiwa kupambana na Inter Milan na Juventus kuwania saini ya beki wa Monza Mbrazil, Carlos Augusto, mwenye umri wa miaka 24. ***(Clciomercato)***


#### YAMFUATA SCHMADTKE

LIVERPOOL ipo kwenye mazungumzo juu ya kumteua Mjerumani Jorg Schmadtke kuwa mkurugenzi wao mpya wa michezo. ***(Mail)***

#### FULHAM YAMTAKA SILVA

KOCHA wa Fulham, Marco Silva, ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni sita katika mkataba wake, huku West Ham akionesha nia ya kumtaka Mreno huyo mwenye umri wa miaka 45 iwapo wataamua kumfuta kazi David Moyes mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA YATWAA TAJI LA KWANZA BILA MESSI

**BARCELONA,** Hispania

●●● Ni hisia nzuri, moja ya kufanya kazi vizuri, alisema Xavi baada ya kutwaa taji hilo na...

BARCELONA imetawazwa kuwa bingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2019 baada ya kushinda mabao 4-2 wakiwa ugenini dhidi ya Espanyol katika mchezo wa dabi ya Katalunya, Jumapili.

**Robert Lewandowski alifunga mabao mawili huku Alex Balde na Jules Kounde kila mmoja akifunga moja.**

Ushindi huo uliifanya Barca kuongoza kwa pointi 14 mbele ya Real Madrid wanaoshika nafasi ya pili na kutwaa ubingwa huo wakiwa wamesalia na michezo minne.

Ni mara ya 27 kwa 'Blaugrana' hao kushinda taji la Ligi Kuu Hispania - ni Madrid pekee ndio wameshinda mara nyingi zaidi (35) - na la kwanza tangu Xavi Hernandez achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo mwaka 2021.

"Ni hisia nzuri, moja ya kufanya kazi vizuri," alisema Xavi baada ya ushindi huo.

"Hii ilianza Julai. Ni miezi 10 ya kufanya kazi kwa bidii na kujitolea. Ilionekana kama wakati wa usiku wa leo (juzi). Kumekuwa na ukosoaji kuhusu kuwapa wachezaji siku tano za mapumziko jambo ambalo halikuwa sawa, lakini lilitusaidia vema.

"Mashabiki wanastahili hili. Wachezaji pia. Pia kumekuwa na jitihada kubwa kutoka kwa rais kujenga kikosi imara.

"Kushinda ubingwa ikiwa imesalia mechi nne kunaonyesha tumekuwa na nguvu zaidi kuliko michezo mingine yote.

"Nina furaha sana, ninajivunia kushinda taji la ligi."

Barca ilishinda ligi mara nane kati ya 2009 na 2019 kama sehemu ya enzi ya dhahabu iliyoongozwa na Lionel Messi, lakini haikufanikiwa kushinda katika misimu mitatu iliyopita.

Mwaka jana, kwa mara ya kwanza wakiwa bila Messi kufuatia kuhamia Paris Saint-Germain, iliwafanya kumaliza kampeni hiyo kwa pointi 13 nyuma ya Madrid waliobuka mabingwa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 583

MECHI KALI
INTER
VERSUS
AC MILAN
1 | 2.01
X | 3.20
2 | 3.56

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP NA MABAO ZAIDI KWA NUNEZ



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza kuwa fowadi Darwin Nunez angefunga mabao mengi zaidi kama Liverpool wangefanya vema zaidi msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, aliyesajiliwa kutoka Benfica majira ya joto kwa kitita cha pauni milioni 84 ambacho ni rekodi ya klabu, amezifumania nyavu mara 15 katika msimu wake wa kwanza.

Hata hivyo, kutokana na takriban wachezaji wote wa kwanza wa Klopp kupatikana tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 amepata shida kupata nafasi kwenye timu, akianza mara tano tu katika mechi 11 zilizopita, amefunga mara moja tu.

Lakini Klopp alisema kushindwa ni kwa timu hiyo, ambayo imekuwa ikitofautiana sana kabla ya ushindi wao wa sasa wa mechi sita, na si mchezaji.

"Kuna mengi zaidi yajayo. Hilo liko wazi. Anahitaji muda kutulia," alisema Klop.

"Kitu kigumu zaidi kwa mshambuliaji. Fikiria kama tungecheza kwa ajili yetu msimu mzuri, msimu wa pointi 80 au zaidi, bila shaka angefunga mabao zaidi.

"Lakini ni kama sasa kila hali tuliyotengeneza na kukosa ni kiwango cha juu zaidi.

"Mo Salah, katika msimu wake bora alipofunga mabao 40. Hiyo ni kawaida. Erling Haaland alipoteza nafasi. Lakini walikuwa na mengi zaidi kuliko tulivyounda katika kipindi hiki.

"Mabao 15 ni sawa kabisa. Bado mechi tatu zimesalia ili aweze kuongeza idadi hiyo pia.

"Alikuwa na wakati wa kuzoea Benfica na hakukuwa na suala la lugha, au chini ya ilivyo hapa. Tulijaribu kumsaidia ili aweze kutusaidia hata zaidi ya alivyofanya tayari."



# Arteta aomba radhi mashabik

**LONDON,** England

MIKEL Arteta aliyechanganyikiwa aliomba radhi kwa mashabiki wa Arsenal baada ya kufungwa mabao 3-0 nyumbani na Brighton na kukatisha matumaini yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Julio Enciso, Deniz Undav na Pervis Estupinan yaliwapatia 'Seagulls' hao ushindi unaostahili pale Emirates, hiyo ikiwa na maana kwamba Manchester City wanahitaji ushindi mmoja zaidi kutoka kwa michezo yao mitatu ya mwisho ili kutetea taji lao.

City wanaweza kuwa mabingwa Jumamosi usiku ikiwa Arsenal watapoteza huko Nottingham Forest huku pengo kati ya timu mbili za juu sasa zikiwa ni pointi nne na vijana wa Pep Guardiola wakiwa na mchezo mkononi.

"Hisia tofauti kabisa na hisia ambazo sote tulikuwa nazo Jumapili iliyopita (huko Newcastle) tulipojisikia faha-

ri na tulihisi kwamba tulifa… ya kile tulichohitaji kushin… katika nyakati fulani. Leo … kinyume kabisa," Arteta a… kiri.

"Tunapaswa kuomba ms… maha kwa watu wetu, hasw… kwa kipindi cha pili.

"Ninachopaswa kukikub… li kwanza ni kile kilichotok… kipindi cha pili na kuyatafa… ari.

"Baada ya hapo hadi kihe… abu kiishe ... nafasi ya pili il… salama. Hilo halitabadilik… Tunapaswa kuchimba … hiyo itachukua siku chache…

,071,860

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/05/23 | 18:00 | Marumo Gallants FC vs Young Africans | 2.50 | 3.30 | 2.50 |
| 02. 17/05/23 | 19:00 | AEL Limassol vs Karmiotissa | 2.69 | 3.27 | 2.48 |
| 03. 17/05/23 | 19:30 | IF Karlstad Fotboll vs Hammarby Talang FF | 2.29 | 3.59 | 2.53 |
| 04. 17/05/23 | 20:00 | Ankaragucu vs Antalyaspor | 2.28 | 3.41 | 2.83 |
| 05. 17/05/23 | 21:30 | National Bank vs Ismaily SC | 2.39 | 2.95 | 3.05 |
| 06. 17/05/23 | 21:35 | Airdrieonians vs Hamilton | 2.45 | 3.23 | 2.66 |
| 07. 18/05/23 | 02:00 | Sport Recife vs Sao Paulo | 2.80 | 2.96 | 2.47 |
| 08. 18/05/23 | 02:30 | Toronto FC vs NY Red Bulls | 2.37 | 3.26 | 2.94 |
| 09. 18/05/23 | 03:30 | America Mineiro MG vs Internacional | 2.56 | 3.01 | 2.65 |
| 10. 18/05/23 | 22:00 | AZ Alkmaar vs West Ham | 2.68 | 3.24 | 2.51 |
| 11. 18/05/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Juventus | 2.35 | 3.14 | 2.98 |
| 12. 19/05/23 | 03:00 | Arsenal Sarandi vs Independiente | 2.90 | 2.85 | 2.47 |
| 13. 19/05/23 | 19:00 | Hillerod vs HB Koge | 2.44 | 3.13 | 2.62 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 16/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1194 | Alashkert Martuni vs Bkma Yerevan | 1.41 | 4.17 | 6.67 |
| 15:00 | 3901 | Legetafo Legedadi vs Fasil Kenema | 4.15 | 3.21 | 1.83 |
| 17:00 | 1261 | Pendikspor vs Bandirmaspor | 1.78 | 3.59 | 3.69 |
| 17:00 | 1347 | AS Khroub vs ES EL Ghozlane | 1.48 | 3.69 | 6.44 |
| 17:00 | 1729 | MC EL Eulma vs CA Batna | 1.61 | 3.52 | 5.18 |
| 17:00 | 1854 | NRB Teleghma vs JS Bordj Menaiel | 5.20 | 3.64 | 1.58 |
| 17:00 | 1954 | Goeztepe vs Caykur Rizespor | 2.73 | 3.29 | 2.27 |
| 17:00 | 2918 | Boluspor vs Eyupspor | 4.63 | 3.70 | 1.60 |
| 17:00 | 3019 | Samsunspor vs Bodrumspor | 1.92 | 3.39 | 3.39 |
| 17:00 | 4237 | Ib Khemis El Khechna vs Hamra Annaba | 1.21 | 5.21 | 12.50 |
| 17:00 | 4356 | Genclerbirligi vs Sakaryaspor | 2.18 | 3.38 | 2.81 |
| 17:00 | 4379 | Tuzlaspor vs Manisa BBSK | 3.89 | 3.59 | 1.74 |
| 17:00 | 5478 | Altinordu vs Erzurum BB | 1.96 | 3.39 | 3.28 |
| 17:00 | 5567 | Irb Ouargla vs Ain M'lila | 1.72 | 3.27 | 4.67 |
| 17:00 | 5699 | Haras EL Hodood vs Arab Contractors | 4.22 | 3.06 | 1.92 |
| 17:00 | 5996 | Sivasspor vs Kasimpasa | 1.98 | 3.48 | 3.42 |
| 18:00 | 2538 | FK Auda vs FC Riga | 7.69 | 4.16 | 1.37 |
| 18:00 | 3271 | Moss vs Aasane Fotball | 2.10 | 3.38 | 2.97 |
| 18:00 | 5877 | Dire Dawa Kenema FC vs Ethiopian Medhin | 2.70 | 3.11 | 2.45 |
| 18:30 | 5542 | Uhersky Brod vs Viktoria Otrokovice | 2.42 | 3.47 | 2.51 |
| 18:40 | 4144 | Al Qadisiyah vs Ohud Medina | 1.92 | 3.03 | 3.85 |
| 19:00 | 1059 | IK Start vs Sandnes Ulf | 1.72 | 3.76 | 3.81 |
| 19:00 | 1082 | Kongsvinger IL vs Skeid Fotball | 1.85 | 3.50 | 3.50 |
| 19:00 | 2079 | Valerenga vs Ham-Kam | 1.70 | 3.68 | 4.42 |
| 19:00 | 2316 | Mjondalen vs Raufoss | 2.33 | 3.34 | 2.62 |
| 19:00 | 2321 | Sogndal vs Hodd | 1.85 | 3.44 | 3.59 |
| 19:00 | 2444 | Kristiansund vs Ranheim | 1.72 | 3.64 | 3.94 |
| 19:00 | 3266 | Stromsgodset vs Sandefjord | 1.82 | 3.63 | 3.84 |
| 19:00 | 3506 | Lillestrom vs Sarpsborg | 1.84 | 3.61 | 3.77 |
| 19:00 | 3527 | Fredrikstad vs Kfum Oslo | 1.93 | 3.43 | 3.33 |
| 19:00 | 3528 | Forde vs Floro | 2.00 | 3.81 | 2.88 |
| 19:00 | 3762 | Rosenborg vs Haugesund | 1.61 | 3.73 | 5.15 |
| 19:00 | 3934 | Viking vs Odd Ballklubb | 1.70 | 3.79 | 4.32 |
| 19:00 | 4628 | Brann vs Stabaek | 1.29 | 5.05 | 8.83 |
| 19:00 | 5029 | Bryne vs Jerv | 2.16 | 3.34 | 2.88 |
| 19:00 | 5069 | Tromso vs Bodo Glimt | 4.63 | 3.79 | 1.65 |
| 19:00 | 5092 | Aalesunds vs Molde | 5.15 | 3.89 | 1.58 |
| 19:00 | 5976 | Smouha Club vs Coca Cola | 3.63 | 3.12 | 2.04 |
| 19:05 | 5144 | AL Akhdood vs AL Qaisoma | 1.57 | 3.64 | 5.03 |
| 20:00 | 3393 | Istanbulspor vs Galatasaray | 6.53 | 4.84 | 1.38 |
| 20:00 | 3660 | Alanyaspor vs Konyaspor | 2.43 | 3.42 | 2.63 |
| 20:00 | 4212 | Orebro SK vs Orgryte IS | 2.09 | 3.35 | 3.40 |
| 20:30 | 2138 | Mamelodi Sundowns vs Maritzburg Utd | 1.50 | 3.98 | 5.86 |
| 21:30 | 1205 | AL Tai vs Al Nasr Riyadh | 5.95 | 4.89 | 1.43 |
| 21:30 | 1987 | Al Hilal Riyadh vs Al Ittihad Jeddah | 2.43 | 3.53 | 2.67 |
| 21:30 | 4398 | Talaea El Gaish vs Farco FC | 2.27 | 2.81 | 3.46 |
| 21:35 | 2940 | Annan Athletic vs Clyde | 2.21 | 3.28 | 2.97 |
| 22:00 | 1773 | Luton Town vs Sunderland | 2.00 | 3.24 | 3.54 |
| 22:00 | 3957 | Inter vs AC Milan | 2.01 | 3.20 | 3.56 |
| 23:30 | 5050 | Academia Cantolao vs Sport Boys Association | 2.21 | 3.23 | 2.87 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# COASTAL UNION YAZIPIGA MKWARA AZAM, SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu juzi kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Klabu ya Coastal Union, imesema itahakikisha inashinda mechi mbili zilizobaki dhidi ya Azam FC na Simba ili kupata pointi sita ambazo zitaihakikishia kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara bila kwenda kucheza mechi za mchujo 'play off.'

Msemaji wa klabu hiyo, Miraji Wandy, amesema wanaziheshimu Azam na Simba kwa sababu ni timu kubwa na ngumu, lakini wao wamejipanga kuhakikisha wanakamilisha kazi ambayo wanachama na mashabiki wa Coastal wamewatuma, kuhakikisha kuwa timu yao inaendelea kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

**"Ni kweli ligi safari hii ni ngumu sana, michezo iliyosalia Coastal Union tulijipanga kuhakikisha tunapata ushindi, imebaki nyumbani dhidi ya Azam na ugenini dhidi ya Simba, tunaziheshimu sana timu hizo, lakini tutahakikisha tunapata ushindi kwenye mechi hizo kama ambavyo huwa tunapata kwenye timu zingine.**

"Tunaanza na Azam FC ambaye anatufuata nyumbani, huku atapigika tu kwa sababu ni mechi ambayo mashabiki wanajazana uwanjani kutupa sapoti kubwa na kutushangilia, na itakuwa ya kuagana kwa sababu hatutaonana tena hadi mwakani. Itakuwa kama sherehe, hivyo Azam ajipange, halafu tunakwenda Dar es Salaam kumalizana na Simba," alisema.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fikiri Elias, aliwashukuru wachezaji wake, kwani wamecheza kwa nidhamu kubwa kiasi cha kupata ushindi huo muhimu.

"Tunashukuru wachezaji wetu walikuwa na nidhamu kubwa kwenye ukabaji, katikati tulimiliki sana mchezo, tulikuwa na mchezo mzuri sana, tulipata nafasi nne tumetumia moja. Tulijua kuwa Ihefu wana timu nzuri sana, sasa tufanyaje ili tushinde, tumiliki mpira na tukimbie zaidi kuliko wao," alisema kocha huyo.

Akizungumzia mechi zinazofuata alisema ni muhimu kwao kushinda ili waende kucheza mechi za 'play off.'

Kwa matokeo hayo, Coastal Union imefikisha pointi 33 ikiwa kwenye nafasi ya 10 ambayo bado haijaipa uhakika wa moja kwa moja kuepuka mechi za mchujo, Ihefu ikiwa juu kwenye nafasi ya tisa kwa pointi hizo hizo 33.

## Nabi ataja mbinu kuimaliza Marumo

INATOKA UK. 23

ya ushambuliaji ya Marumo katika kutengeneza nafasi.

"Marumo Gallants si timu mbaya kwa sababu washambuliaji wake ni wazuri, mechi ya kwanza waliweza kutusumbua, lakini safu yao ya ulinzi inashida, tukiweza kutumia madhaifu yao tutarejea nyumbani tukiwa tunacheza fainali, lakini tusipokuwa makini tutaweza kupoteza hii mechi," alisema Nabi.

Aidha, kocha huyo alisema kukosekana kwa nyota wake, Bernard Morrison, kwenye mchezo huo hakutaathiri kitu chochote kwa sababu ya kuwa na kikosi kipana hususan mbadala.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema wamefika salama na wachezaji wote wapo salama na tayari kwa mchezo huo.

"Tumefika salama, timu imefanya mazoezi katika uwanja uliopo katika hoteli tuliyofika, kazi iliyopo sasa ni wachezaji kufuata yale wanayoelekezwa na kocha ili kuhakikisha tunafanikiwa kucheza fainali ya Afrika," alisema Kamwe.

## MTOTO UMLEAVYO...



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lumumba, wakicheza mpira katika viwanja vya JMK Park jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE JUMA

## Robertinho amaliza kazi

INATOKA UKURASA 24

chao msimu ujao.

Alisema kulingana na ukubwa na wachezaji wazuri walipo ndani ya Simba mashabiki wao watasikia mambo mengi kuhusu baadhi ya nyota kutakiwa kuondoka au kusajiliwa na klabu zingine.

"Hakuna ukweli juu ya nyota hao, tunatambua Manula aliumia na yuko kwenye matitabu, Chama na Tshabalala bado wataendelea kuonekana uwanjani, mashabiki wanapaswa kuelekeza nguvu katika mechi mbili zilizosalia kwenye ligi kuliko hizi taarifa za kututoa katika mstari," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa nyota hao wawili wako katika kikosi cha Simba na wanaendelea na maandalizi ya michezo miwili iliyosalia ya Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania utakaopigwa Mei 24, katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kabla ya kuhitimisha msimu uwanjani hao dhidi ya Coastal Union Mei 28, mwaka huu.

# Michezo

Jumanne Mei 16, 2023

Nipashe




Barca yatwaa taji bila Messi UKURASA 21

HAPA MWISHO...




Beki wa kati wa Brighton, Lewis Dunk, akimdhibiti mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus (kushoto), kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi usiku na kumalizika kwa wageni hao kushinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# *Robertinho apewa rungu, akabidhi majembe Simba*

## ●●● Ashirikiana na jopo la wataalamu wa usajili baada ya uongozi...

**Na Saada Akida**

BODI ya Wakurugenzi ya Simba chini ya Mwenyekiti wake, Salim Abdallah (Try Again), imesema imekabidhi majukumu yote ya usukaji kikosi kipya kwa ajili ya msimu ujao kwa Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira pamoja na wataalamu wengine wa mambo ya usajili na tayari shughuli imeanza kwa kufikishiwa majina ya wachezaji anaowataka.

Simba imedhamiria kusuka kikosi imara kuelekea msimu mpya hususan kwa ajili ya michuano ya Super League, ikiwa ni timu pekee kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki itakayoshiriki kipute hicho kinachotarajiwa kushirikisha klabu kubwa nane barani Afrika kuanzia Oktoba mwaka h Akizungumza na Nipashe jana, Try Again alisema tayari Robertinho ameshapendekeza nafasi na majina ya wachezaji wapya ambao anawahitaji kwa msimu ujao ili kuimarisha timu hiyo kuwa na kikosi imara.

**Alisema wamempa jukumu la usajili Robertinho ambaye atashirikiana na wataalamu wengine wa mambo ya usajili kufanya kazi hiyo ikiwamo kuangalia wachezaji wanaostahili kubaki kikosini na kupendekeza wapya wanaomfaa kulingana na mfumo wake jambo ambalo tayari amelifanyia kazi katika ripoti yake ya awali.**

"Kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na maingizo mapya ya wachezaji msimu ujao, wenye maono ya kutufikisha pazuri katika michuano ya kimataifa, lakini kwa sasa kazi kubwa ni kuboresha na kuongezea mikataba kwa wachezaji wetu ambao wanatakiwa kusalia ndani ya kikosi cha msimu ujao," alisema Try Again.

Alisema baada ya kutopata taji lolote msimu huu wamedhamiria kufanya maamuzi magumu katika mabadiliko ya kikosi chao kwa kusajili wachezaji ambao wataifikisha Simba katika malengo yanayotarajiwa na mashabiki.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya kama bodi kwanza tutaangalia tathmini na ripoti ya kocha kwa viwango vya wachezaji, lakini jukumu la usajili mpya tayari mwalimu amefanyia kazi na kuleta maji au nafasi ya watu wake anaotaka kufanya nao kazi kwa msimu ujao," alisema Try Again.

Alisema wako katika kuboresha kikosi kwa sababu wanahitaji kufanya vizuri zaidi katika michuano ya msimu ujao ikiwamo Super League ambayo Simba imekuwa ni timu pekee kwa Ukanda wa CECAFA kushiriki kombe hilo la timu nane kubwa Afrika.

Wakati huo huo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, aliwataka mashabiki kuachana na taarifa za nyota wao watatu muhimu, Clatous Chama, Aishi Manula na Mohammed Hussein 'Tshabalala' kuwa hawatakuwa sehemu ya kikosi

INAENDELEA UKURASA 23

# Nabi ataja mbinu za kuimaliza Marumo

**Na Saada Akida**

WAKATI kesho akitarajia kukiongoza kikosi chake katika Uwanja wa Royal Bafokeng uliopo Rustenburg, Afrika Kusini kuivaa Marumo Gallants kwenye mechi ya mkondo wa pili ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema itakuwa ni mechi ngumu hasa dhidi ya timu hiyo ikiwa nyumbani, lakini akataja mbinu zake atakazotumia kutinga fainali.

Yanga inahitaji sare yoyote ama kutokubali kufungwa zaidi ya bao moja ili kutinga fainali ya michuano hiyo na kuandika rekodi ya klabu, tangu kuanzishwa kwake miaka 88 iliyopita.

Hiyo ni kutokana na kushinda nusu fainali ya kwanza Jumatano iliyopita kwa mabao 2-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema kwa sasa anaendelea kuwaongezea wachezaji wake umakini na kutumia vema nafasi wanazotengeneza ili kutafuta bao la mapema katika ardhi ya Afrika Kusini jambo litakalowachanganya Marumo Gallants.

Alisema anajua ubora wa wapinzani wao wanapokuwa nyumbani na wanahitaji kutumia madhaifu yao hasa katika safu yao ya ushambuliaji kutafuta bao la mapema katika kipindi cha kwanza.

Alisema ameona madhaifu ya mpinzani wao huyo hasa katika safu ya ulinzi, lakini akiwataka mabeki wake kuwa makini kutokana na uwezo wa safu

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >